# Nipashe

Alhamisi Aprili 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580544

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.faceb… …ipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Diwani** akutwa amefariki dunia nyumba ya wageni

UKURASA 3



**Bei** za petroli, dizeli zazidi kupanda nchini

UKURASA 4




**Ibrahimovic apewa mkataba mpya AC Milan**

UKURASA 21

# Wabunge wataja siri ya kishindo cha Rais Samia

UKURASA 2





Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na viongozi wengine wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wakiomba dua mbele ya kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume katika Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui Zanzibar jana, katika kuadhimisha Siku ya Karume. **Picha zaidi Uk. 7. PICHA: IKULU**

## Samia, Mwinyi waongoza kisomo dua ya Karume

UKURASA 3

## Wadau washangaa kigugumizi kufunguliwa vyombo vya habari

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **NTIBAZONKIZA: YANGA ITANG'ARA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mazishi ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu kufikia mwisho wa maombolezo ya kitaifa ya kifo hicho, kilichotokea machi 17, mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge wataja siri kishindo cha Samia

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wametaja wanachokiamini kuwa ndicho siri ya kung'ara kwa Rais Samia Suluhu Hassan, muda mfupi baada ya kushika madaraka hayo ya juu zaidi nchini.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jijini Dodoma, wabunge hao walisema sababu za kung'ara kwa Rais Samia ni pamoja na kuwa sehemu ya uongozi wa juu wa serikali kwa takribani miaka sita, hivyo kuwa mzoefu wa kazi.

Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), alisema Rais Samia ni kiongozi shupavu anayejiamini na ameonyesha hayo kwa kishindo ndani ya muda mfupi aliokaa katika nafasi ya urais tangu kuapishwa kwake Machi 19, mwaka huu.

Alisema Rais Samia hajatokea kama uyoga, bali ni kiongozi aliyelelewa kwenye tanuri la viongozi na hajapata nafasi hiyo kwa bahati mbaya. Hivyo kutokana na uwezo alionao, hivyo watu wasiwe na wasiwawasi naye.

Msambatavangu alisema anamfahamu vizuri Rais Samia tangu akiwa kwenye nafasi mbalimbali ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Waziri na Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba pamoja na Makamu wa Rais na kote huko alionyesha uwezo mkubwa.

Mbunge huyo alisema Rais Samia ameonyesha ni mzoefu wa uongozi kwa siku chache tangu ashike madaraka ya urais kutokana na kufanya uteuzi wa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ambaye watu wengi hawakutegemea.

"Unajua moja ya sifa ya kiongozi ni kufanya mabadiliko, na pale unapokuta umekosea, unaendelea kurekebisha hapo hapo bila kuogopa maneno ya watu. Viongozi wengine wakikosea, wanaona aibu kutengua, lakini Rais Samia ameonyesha ukomavu kwa kufanya mabadiliko kwa haraka bila woga wowote," alisifu.

Mbunge huyo alisema kuwa kutokana na nafasi aliyopata, wapo watakaomsifu kinafiki na wengine kumbeza, lakini ni Rais ameonyesha kuwa ni mchapakazi kutokana na uwezo alioonyesha kwa siku chache tangu akabidhiwe kuongoza nchi.

Alisema kuwa ameonyesha njia na Rais mwenye msimamo na ameahidi kuendeleza yale mazuri yaliyoachwa na mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli.

"Lakini, Rais ndani yake ni mama. Kwa hiyo, wanasema rehema ya mama ina huruma kuliko ya baba, ambacho tunakitegemea ataangalia pale ambapo mengine yalifanyika na watu wengine waliumizwa, wanategemea mama ayarekebishe," alisema.

**ELIBARI KINGU**

Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu (CCM), alisema kuwa akiwa ni miongoni mwa vijana, anaona nchi inakwenda vizuri kutokana na aliyechukua madaraka, alishiriki katika Hayati Dk. Magufuli.

Alisema watu wengi wameshangazwa na uongozi wa Rais Samia kufanya mambo makubwa ndani ya muda mfupi licha ya hofu iliyokuwapo iliyochagizwa na mila na desturi za kiafrika kushindwa kuwaamini wanawake katika nafasi za uongozi.

"Rais Samia amejipambanua, ameonyesha ni kiongozi jasiri na hii imeonyesha kuwa CCM ina hazina ya vingozi ambao wameandaliwa nyakati zote, hata ziwe ngumu au nyepesi kwenye kushika madaraka," alisema.

Aliongeza kuwa Watanzania wamepata matumaini kwa muda mfupi na Rais ameonyesha kuanza kuwashughulikia watu wanaotajwa kufanya vibaya kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

SOPHIA MWAKAGENDA

Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda (CHADEMA), alisema amefurahishwa na uteuzi wa Rais Samia, hasa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutokana na kuteua watu wenye uzoefu mkubwa wa kimataifa, watakaomsaidia kuunganisha nchi na jumuiya za kimataifa.

Aliongeza kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashari, Balozi Liberata Mulamula, ana uzoefu wa kimataifa kutokana kufanya kazi nje ya nchi kwa muda mrefu, hivyo atalisaidia taifa kwenye nyanja ya kimataifa.

Mwakagenda alisema kuwa pia amefurahishwa na uteuzi wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akiamini ataendeleza sekta za afya na miundombinu na kuwasiadia wananchi, hasa za kinamama na watoto ambazo zimekuwa zikilalamikiwa.

"Sisemi kuwa waliotangulia walifanya vibaya, hapana! Ila Mwalimu ninajua ataongeza nguvu katika kupambania na kuongeza ushawishi katika ujenzi wa hospitali na zahanati pamoja na huduma bora za afya," alisema.

Samia aliapishwa kuwa Rais wa Tanzania Machi 19 mwaka huu, ikiwa ni siku mbili baada ya kutangazwa kwa kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. Magufuli, kilichotokea katika Hospitali ya Mzena mkoani Dar es Salaam alikokuwa anatibiwa maradhi ya moyo.

# Wadau washangaa kigugumizi kufunguliwa vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU mbalimbali wa habari wamemjia juu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbasi, kuhusu kauli yake juu ya utekekezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

Juzi, Rais Samia aliagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyofungiwa lakini muda mfupi baadaye, Dk. Abbasi alisema wameagizwa kufungulia TV mtandao na si magazeti.

Kutokana na kauli yake hiyo, baadhi ya wadau wamehoji juu ya uelewa wa vyombo vya habari ambavyo vimetakiwa kufunguliwa huku wakienda mbali zaidi kwamba kufanya hivyo, kama alivyodai Dk. Abbasi, ni kuendeleza ubaguzi dhidi vyombo vya habari na uhuru wake kwa ujumla.

Katika ukurasa wake wa twitter, Katibu wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, aliandika: "Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Dk. Hassan Abbasi, bado ana 'hamu' ya kuendelea kufungia magazeti kwa kutafsiri maelezo ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan eti amri yake inahusu kufunguliwa kwa Online TV tu... Ndugu yetu huyu hajifunzi."

Naye Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, aliandika katika ukurasa wake wa twiter: "Uamuzi wa Katibu Mkuu Habari, Dk. Hassan Abbasi, kulipa tafsiri finyu agizo la Rais SSH la kufunguliwa kwa vyombo vya habari (anadai hajaagizwa kufungulia magazeti, ni Online TV tuu) ni dalili kuwa kichwani mwake bado anaishi zama za mtangulizi."

Alisema: "Katika muktadha ambao Rais SSH alikuwa anazungumzia uhuru wa vyombo vya habari, Dk. Abbasi alipaswa kuchukua Online TV kuwa ni mfamo tu wa vyombo vingi vya habari vilivyofungiwa.

"Bila shaka, kinachompa ukakasi Dk. Abbasi ni kuwa alikuwa sehemu (kama siyo kinara) wa kufungia vyombo vya habari vyenye kukosoa serikali na kuviacha vitambe vyombo vyenye kusifia serikali hata kama vilikuwa vikikiuka miiko ya uandishi na haki binafsi za watu."

Akihojiwa juzi na Wasafi TV baada ya kuapishwa kushika nafasi hiyo, alisema: "Kwanza ni agizo la Amiri Jeshi Mkuu, ni Rais na ni Amiri Jeshi Mkuu, ila pale ame 'specify' kabisa kuna Online Tv zimefungiwa na unafahamu amefanya mageuzi Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kwa hiyo cha kwanza leo leo (juzi) tutaenda kuona ni Online TV gani zilifungiwa kwa sababu gani na kuchukua hatua kama alivyoelekeza," alisema na kuongeza:

"Alisisitiza vyombo viendelee kuzingatia maadili, sheria za nchi, lakini kwa hivi alivyoagiza tunakwenda kuchukua hatua moja kwa moja. Tutaiona hiyo orodha ni ipi na tutatoa kwa umma ili watu wajue ni TV gani zimeachiwa.

"Leo ame- 'specify' kwenye Online TV tutalifanyia kazi hilo, lakini kama kuna maelekezo mengine pia tutachukua hatua kama 'goodwill' (nia njema) ambayo anaitoa watu wandelee kufanya kazi zao lakini kuzingatia sheria,"alisema na kuongeza;

"Hilo (la magazeti) hakulisema lakini kwa sababu amezungumzia kwenye Online TV hilo tunaenda kulifanyia kazi leo (juzi) lakini kama kutakuwa na maelekezo mengine pia sisi ni watekelezaji, sisi ni timu tunatekeleza." Alisema.

Taarifa ya Ikulu iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, alisema rais ameagiza vyombo vilivyofungiwa vifunguliwe na kutakiwa kuzingatia sheria.

Juzi Rais Samia akizungumza na viongozi mbalimbali mara baada ya kuwaapisha makatibu wakuu na manaibu aliowateua pamoja na wakuu wa taasisi, aliagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari na kuhakikisha vinafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na siyo kuviadhibu kwa kutumia ubabe.

"Kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.....mmhhh...? huku nina mengi. Lakini ni kusimamia vyombo vya vyetu vya habari vya ndani," alisema Rais Samia.

"Na nasikia kuna vijivyombo vya habari huko mlivifungia fungia, sijui viji TV vya mikononi vile. Vifungulieni lakini wafuate sheria na miongozo ya serikali. Vifungulieni tusiwape mdomo wa kusema tunabinya uhuru wa vyombo vya habari."

"Lakini mhakikishe kila mliyempa ruhusa ya kuendelea na chombo cha habari anafuata sheria za serikali na kanuni ziwe wazi. Kosa hili adhabu yake ni hii na mnakwenda kwa adhabu mlizoziweka kwenye kanuni. Tusifungie tu kibabe, wafungulieni lakini tuhakikishe wanafuata kanuni na miongozo ya serikali."

Magazeti yaliyo kifungoni ni Mawio na Mwanahalisi huku Tanzania Daima ikifutwa kabisa.

## HABARI KITAIFA

# Diwani akutwa amefariki dunia gesti

**Na Dotto Mwaibale**

DIWANI wa Kata ya Mbagala Kuu, Shabani Othman Abubakari, amefariki dunia katika moja ya nyumba ya kulala wageni Mbagala Zakhem, jijini Dar es Salaam, akidaiwa kuwa na mwanamke.

Taarifa za kifo chake zimethibitishwa na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke, Abdallah Mtimika na kuwa mazishi yake yamefanyika jana katika makaburi ya Tanita, eneo la Kibonde Maji.

Mmoja wa wahudumu nyumba hiyo ya kulala wageni (jina linahifadhiwa), alisema diwani huyo alifika akiwa na gari lake na mwanamke huyo usiku wa kuamkia juzi na kuchukua moja ya chumba katika nyumba hiyo.

Alisema asubuhi baada ya kuamka wakati akifanya usafi alikuta ufunguo wa chumba alichokuwa amekichukua ukiwa umetupwa chini hali iliyomfanya ashtuke na kwenda katika chumba hicho ambacho kilikuwa kimefungwa.

Alisema kilipofunguliwa walimkuta diwani huyo akiwa amefariki, lakini mwanamke aliyekuwa naye hakuwapo.

Mhudumu huyo alisema walitoa taarifa polisi ambao walifika na baada ya kuwahoji waliuchukua mwili wa marehemu kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Jitihada za kumpata Kamanda wa Polisi Mkoa wa Temeke ili kuzungumzia suala hilo ziligonga mwamba baada ya kupigiwa simu yake mara kadhaa na kuita bila ya kupokelewa.



Kinamama wakisubiri kuwaosha miguu wateja wanaotoka nje ya soko la ndizi la Mabibo maarufu kama Mahakama ya Ndizi, mkoani Dar es Salaam jana, kutokana na soko hilo kuwa na tope jingi hasa kipindi hiki cha mvua. Gharama ya kuosha inaanzia 200/- hadi 500/- kwa mtu mmoja. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia, Mwinyi waongoza kisomo dua ya Karume

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

VIONGOZI wa kitaifa wakiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, na rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wameongoza wananchi katika kisomo cha dua kumuombea Rais wa kwanza wa Zanzibar, Sheikh Amani Abeid Karume, aliyefariki dunia Aprili 7, mwaka 1972.

Mzee Karume aliuawa kwa kupigwa risasi katika ofisi kuu ya CCM Kisiwandui mjini Unguja.

Kisomo cha dua kiliongozwa na Katibu wa Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Khalid Mfaume, ambaye alimuelezea Mzee Karume kuwa ni kiongozi aliyeweka alama ya ukumbusho mkubwa kwa wananchi wake wa Unguja na Pemba.

Alisema katika kipindi cha miaka tisa cha uongozi wake alifanya mambo makubwa ya kujenga ustawi wa wananchi wake, ambao unakwenda sambamba na malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Naye Sheikh Shaaban Batwashi kutoka Baraza la Maulama Zanzibar, alisema Hayati Karume katika uhai wake aliongoza kwa kufuata misingi ya haki, usawa na kuona wananchi wake wanapiga hatua kubwa ya maendeleo.

Aliwataka wananchi kuendelea kumuombea dua kiongozi huyo na kuyakumbuka mambo mazuri aliyoyafanya katika uhai wake, ambayo yalilenga kuleta mabadiliko makubwa kwa maslahi ya wananchi.

Mapema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliongoza kuweka shada la maua katika kaburi la kiongozi huyo na kufuatiwa na Rais Samia.

Nae, Mkuu wa majeshi ya ulinzi na usalama, Jenerali Venance Mabeyo, aliweka shada la maua katika kaburi akifuatiwa na kiongozi wa familia ya Hayati Karume, Balozi Ali Karume ambaye ni mtoto wa pili wa mzee Karume.

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Kabi, alisema Hayati Karume alisema kwamba hatokwenda kufanya ibada ya Hijja Makka hadi atakapoona wananchi wake wanaishi katika makazi bora yenye stara.

Alisema hayo wakati akitoa mawaidha ya kumuombea dua Hayati Abeid Karume.

Alisema kilichofanywa na hayati Karume kilikuwa sahihi kwa sababu alitaka kuwafanyia mambo mazuri yanayostahiki kufanyiwa wananchi kutoka kwa kiongozi wao.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake, alifanya kazi kubwa ya kujenga nyumba za ghorofa katika visiwa vya Unguja na Pemba hadi vijijini kwa maslahi ya wananchi wake kuona wanaishi na kulala sehemu bora inayostahiki.

"Hayati Sheikh Karume alisikika akisema kwamba hatokwenda kuhiji Makka hadi hapo atakapofanikiwa na kuwawezesha wananchi wake waishi katika makazi bora.....wanalala sehemu nzuri," alisema Mufti.

Alisema Hayati Karume alifanya kazi kubwa ya kujenga umoja na mshikamano na maridhiano kwa wananchi wa Zanzibar baada ya Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964 na kuwataka wananchi kusahau yaliyopita na kufunguwa ukurasa mpya wa maisha.

Kwa upande wake Balozi Karume , ambaye aliwahi kuwa Balozi wa Tanzania katika nchi mbalimbali za Ulaya zikiwamo Ubelgiji, Ujarumani, na Italia, alizipongeza serikali zote mbili kwa kuendeleza utaratibu wa kumuenzi kiongozi huyo rais wa kwanza wa Zanzibar, ambaye alifanya kazi kubwa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na kuleta maendeleo.

"Sisi familiya ya watoto wa Hayati Karume tunatoa shukrani za dhati kwa serikali zote mbili kwa kuendelea kumuenzi kiongozi wetu kutokana na mchango wake mkubwa wa kuongoza Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo hadi kifo chake alikuwa makamu wa kwanza wa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Viongozi wengine waliohudhuria ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume na viongozi wengine wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano.


**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**
**LAND CASE REVISION No. 11/2019**
**(Arising from Application No. 34/2012 of Bukoba DLHT)**
**BUKOBA MUNICIPAL COUNCIL ................................................APPLICANT**
**VERSUS**
**KINYATA TINDAMANYILE & 33 OTHERS .................................DEFENDANT**
**TO:**

| | |
|---|---|
| 01. KINYATA TINDAMANYILE | 18. VAILETH L. SIMON |
| 02. ALLI CHAMANI | 19. JONES R. KAZIMOTO |
| 03. JAMALI MUSTAPHA | 20. PETER JOSEPH |
| 04. GORETH DAVID MUHOBUJA | 21. EDITH FRANCE NASIMIRE |
| 05. ERICK APPOLLO KALEMBO | 22. LUCAS R. KAZIMOTO |
| 06. BERNARD JOSEPH | 23. ADRIAN LWEBANGIRA |
| 07. SAMORA GEORGE | 24. RWECHUNGURA DIONIZ |
| 08. PROJEST MUTASHOBYA | 25. GRACE RWEYEMAMU |
| 09. IMERIDA NDAMUGOBA | 26. RUKIA YUSUPH |
| 10. APRONIA JOHN | 27. LEONARD L. JOSHUA |
| 11. PENDO K. ANDREA | 28. JONES K. RWEZAULA |
| 12. LAURENCE M. MUHEMBE | 29. KOKUTONA R. KAMUGISHA |
| 13. JOSEPHINA RUTANUKA | 30. JOERI NATHAN |
| 14. FARIDA ISHENDA YAHAYA | 31. DEOGRATIAS MWOMBEKI |
| 15. MUSWADIKU H. KIGWA | 32. ABUBAKARI ABDALLAH |
| 16. BLANDINA W. NDYAMUKAMA | 33. JANETH J. JOEL |
| 17. ANGERA SALVATORY | 34. G. JAFFER |

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Applicant lodged the Application against you and registered as **Land Case Revision No. 11/2019.**

Take Notice that the above said application has been fixed for mention on **27th April, 2021 at 8:30** Am before Hon. **NTEMI N. KILEKAMAJENGA, J.** You are ordered to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said hearing the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of this Court this **06th day of April, 2021.**

**J. M. Minde**
**DEPUTY REGISTRAR**
**BUKOBA.**

## Wamtumia ujumbe Waziri kuhusu kero

**Na Romana Mallya**

MAELFU wamejitokeza kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, wakimweleza kero mbalimbali wanazokutana nazo hospitalini.

Katika taarifa yake aliyoitoa jana kwa ajili ya shukrani kwa wateja kwa kutoa pongezi, maoni na kero za huduma za afya, Waziri Gwajima aliwataka wananchi waendelee na huduma hiyo ya kutoa taarifa.

Desemba 19, mwaka jana, Waziri huyo alitoa namba yake ya simu 0734124191 ili kutoa fursa kwa wananchi kumtumia ujumbe mfupi pindi wanapokutana na kero wanapoona hawakupata msaada kwenye ngazi ya kituo, halmashauri na mkoa.

"Ninawashukuru maelfu ya wananchi ambao pale au Wizara kupitia namba husika zilizotangazwa mmekuwa mkizingatia kunitumia ujumbe mfupi kwenye simu yangu kama nilivyoitangaza Desemba," alisema.

Waziri Gwajima aliwaeleza wananchi kuwa, kamwe wasikose mahali pa kusemea bali waendelee kutumia mifumo ya mawasiliano ya haraka kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa.

Aliwahakikishia wananchi kuwa ataendelea kujibu na akiona inafaa atapiga simu au kutoa maelekezo kwa wasaidizi wake wafuatilie na kusimamia jambo hilo na kumpa mrejesho.

"Watumishi wataalamu wa afya, natoa pongezi kwa wale wote ambao wamekuwa wakijituma kwa bidii kuwahudumia wateja wanaohitaji huduma za afya. Hakika kupitia maoni ya wateja tumeendelea kuwatambua watumishi wengi wenye moyo wa uzalendo na upendo katika kutimiza wajibu wao," alisema. Alisema wale wenye changamoto nao wameendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni.

Pia aliwashukuru wananchi wote ambao wamekuwa wakiwasilisha pongezi, maoni na kero zao kupitia mifumo mbalimbali ya mawasiliano ya wizara ikiwamo kwa barua, mitandao ya kijamii, simu na ujumbe mfupi kupitia namba 199.

"Nikiri kuwa taarifa hizo zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika kutambua maeneo yanayofanya vizuri na yale yenye changamoto," alisema



Askari Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akikagua ajali ya gari iliyotokea baada ya dereva wake kugonga ukingo wa Barabara ya Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bei za petroli, dizeli zazidi kupaa

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli na dizeli ambazo kwa rejareja zimeongezeka kwa Sh. 142 kwa lita.

Taarifa iliyotolewa jana mkoani Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, ilionyesha bei hizo ambazo zimeanza kutumika kuanzia siku hiyo (Jumatano), kwa rejareja imeongezeka kwa asilimia 7.18 (petrol) na Sh. 85 kwa lita sawa na asilimia 4.46 (dizeli).

Katika taarifa hiyo, Mhandisi Chibulunje alitaja bei ya rejareja kwa mikoa ambapo Dar es Salaam petroli itauzwa Sh. 2,123 kwa lita na dizeli Sh. 1,996 kwa lita.

"Arusha petroli itauzwa Sh. 2,211 kwa lita na dizeli Sh. 2,081 kwa lita, Dodoma petroli Sh. 2,182 kwa lita na dizeli Sh. 2,055 kwa lita, Kilimanjaro petroli itauzwa Sh. 2,201 kwa lita na dizeli Sh. 2,070 kwa lita," alisema.

Alisema bei za rejareja na jumla za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yaliyopokelewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam zimeongezeka ikilinganishwa na toleo la mwezi Machi.

Alisema bei hizo zikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, jumla ya petroli na dizeli zimeongezeka kwa Sh. 141.92 kwa Lita sawa na asilimia 7.66 na Sh. 84.95 kwa lita sawa na asilimia 4.77 mtawalia.

"Bei za mafuta ya taa hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la Machi 3, mwaka huu, hii ni kwa sababu, kwa mwezi Machi hakuna shehena ya mafuta ya taa iliyopokelewa kupitia bandari ya Dar es Salaam," alisema.

Alisema kwa mwezi Aprili, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya petroli na dizeli kwa mikoa ya Kaskazini inayohusisha Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara zimeongezeka ikilinganishwa na bei zilizotolewa mwezi uliopita.

Alisema bei za rejareja za petroli zimeongezeka kwa Sh. 73 kwa lita sawa na asilimia 3.49 na dizeli Sh. 105 kwa lita sawa na asilimia 5.50.

Alisema ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za petroli zimeongezeka kwa Sh. 72.38 kwa lita sawa na asilimia 3.71 na dizeli Sh. 105.12 kwa lita sawa na asilimia 5.87.

"Bei za mafuta ya taa hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la Machi. Hii ni kwa sababu, kwa mwezi huo hakuna shehena ya Mafuta ya taa iliyopokelewa kupitia bandari ya Tanga," alisema.

Alisema kwa mwezi Aprili, bei za rejareja na jumla kwa mafuta ya petroli na dizeli kwa mikoa ya Kusini inayojumuisha Mtwara, Lindi, and Ruvuma, zimeongezeka ikilinganishwa na za mwezi uliopita.

"Bei ya rejareja ya petroli zimeongezeka kwa Sh. 92 kwa lita sawa na asilimia 4.47 na dizeli Sh. 200 kwa lita sawa na asilimia 10.96. Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji," alisema.

Alisisitiza kuwa, ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja kwani adhabu kali itatolewa kwa kituo husika.

# CWT yapata dawa ya mikopo umiza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimesema uwapo wa Benki ya Mwalimu (MCB) ni suluhisho la tatizo la mikopo umiza linaloikabili kada hiyo kwasasa kutokana na kumpa nafasi mwalimu kuwa mwana hisa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu namna ya kuwakomboa walimu kuondokana na adha hiyo, Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alisema benki hiyo ilianzishwa ili kumkomboa mwalimu.

Kwa mujibu wa Deus, lengo ni kuona benki hiyo inamkopesha mwalimu kwa riba nafuu tofauti na benki zingine.

"Hii benki ili ifanye vizuri ni lazima iwe na wateja na wakati tunaanzisha hii benki mteja namba moja tulisema ni mwalimu. Tupo takribani walimu 300,000 na tukasema tukianzisha hawa wote wakatumia benki yao itakuwa imara na itakuwa benki bora nchini, lakini tangu imeanzishwa hawazidi 4,000,"alisema.

Alibainisha kuwa benki hiyo imeanza kutoa huduma bora na za kisasa na kuifanya iwe kimbilio la walimu kwa kuanzisha mfumo rafiki kwa wanahisa wake ambao ni walimu ili kunufaika na benki yao.

"Ukombozi utakaotufanya walimu tusimame ni benki ya walimu na vyama vyote vya wafanyakazi barani Afrika wanashangaa CWT ina benki. Wanauliza mmefanyaje mmeweza, lakini walimu hatulijui hili, walimu warudi kwenye benki yao wao ni wanahisa ni wamiliki wa benki ikipata faida na yeye anapata mgawo,"alisema.

Katibu huyo alisema benki hiyo ni sehemu ya kutatua tatizo hilo na Benki ina fedha hadi zinakosa wakopaji kwa kuwa zililenga zaidi walimu na kuwataka kukopa na kutumia benki hiyo.

"Wengi wanaoumia ni wale wanaokwenda kustaafu. Hao ndio wanaofuatwa, nitoe rai kwa wanaotarajia kustaafu walimu waje MCB kuna vitu vingine wataviona, na Benki inanunua mikopo na utapitisha mshahara sasa kwenye benki yako ya walimu na kama utataka kuongeza mkopo kuna fursa kwa hiyo benki hii ni sehemu ya suluhu,"alisema.

Katika hatua nyingine, CWT imepongeza uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuiagiza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuanza mchakato wa ajira za walimu 6,000 na kwamba hatua hiyo inaonyesha alivyoipa kipaumbele sekta ya elimu na dhamira ya kumpunguzia mzigo mwalimu ili afanye kazi kwa ufanisi.

Katibu huyo alisema chama hicho kitaendelea kumuunga mkono Rais Samia katika mipango yake ya kuboresha zaidi sekta ya elimu nchini ili kuliwezesha taifa lipige hatua kubwa zaidi kimaendeleo.

"Tumeanza kupata ushirikiano na tunaamini tutaendelea kupata ushirikiano zaidi, kitendo cha kutoa replacement ya walimu 6,000, utaona ni kwa namna gani sekta ya elimu tutapata ushirikiano na tumeanza kupata ushirikiano huo," alisema.

Naye, Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Richard Makungwa, alisema walimu 41,000 ndiyo waliojiunga na benki hiyo ambao ni wanachama wa CWT jambo linalosababisha kushindwa kukua kimtaji.

"Asilimia 35 ya wanachama wa CWT wanahisa ndani ya benki, hivyo wakiamua wote kuitumia kama wanavyotumia katika taasisi nyingine za fedha, wanaweza kuikuza benki, tunaendelea kuboresha huduma kwa kuwa lengo ni kumsaidia mwalimu,"alisema.

Kwa miaka miwili iliyopita Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ilirejesha mamilioni ya shilingi kwa walimu na watumishi wa kada zingine, waliokuwa wameingia kwenye mikopo umiza.

## HABARI KITAIFA

# Maaskofu na mapadri wamwelezea Monsinyori Mbiku hakuwa mbaguzi

**Na Romana Mallya**

MAASKOFU na mapadri wameeleza maisha ya Monsinyori Deogratius Mbiku, aliyekuwa Paroko wa Parokia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa katika utumishi wake aliwatumikia watu bila kujali dini zao.

Katika misa ya mazishi iliyofanyika jana Pugu jijini Dar es Salaam, Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thaddeus Ruwa'ichi, alisema Monsinyori Mbiku alikuwa na mwanzo wa kufikirisha.

Adhimisho la misa hiyo liliongozwa na Askofu Mkuu Ruwa'ichi kwa kushirikiana na Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Gervas Nyaisonga ambaye pia ni Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mbeya.

Katika misa hiyo, Askofu Ruwa'ichi alisema Monsinyori Mbiku alizaliwa katika familia ya Kiislam na awali alilelewa kama Mwislam.

"Aliwahi kunishirikisha kwamba baba yake mzazi alitegemea awe kiongozi wa dini ya Kiislam, awe Sheikh lakini Mungu ana mipango na njia zake, alishamwandaa tangu awali kwa mpango wake.

"Akiwa mwanafunzi shule ya msingi alianza polepole kupekua na kujifunza kuhusu Ukristo na hatimaye akaamua kutafuta ubatizo. Halikuwa jambo rahisi kwake wala wazazi wake lakini wazazi wake hawakughairi walimruhusu," alisema.

Monsinyori Mbiku, alisema alikuwa mtumishi wa Mungu, chombo cha imani na shahidi wa imani yake na katika safari yake ya maisha alisikia wito wa upadri na halikuwa rahisi kwa familia yake.

Alisema alipewa daraja la upandre, ameishi kwenye wito wake na aliwahudumia watu wote Wakristo na Waislam.

Akitoa salamu za TEC, Askofu Mkuu Nyaisonga, alisema Monsinyori Mbiku alikuwa kielelezo, aliitwa na aliitika vizuri katika wito wake wa upadri.

"Ametuhudumia katika nyakati na ngazi mbalimbali wasifu wake unathibitisha hayo na kila alipohudumia alidhihirisha wazi uzuri wa upandri na furaha katika kutumikia, alihamasishwa na mapadri aliowaona ututoni naye akawa padri," alisema.

Alisema watamkumbuka kwa namna alivyopenda maandiko matakatifu na alijitahidi maisha yake yawe ushuhuda wa kweli.

Askofu Nyaisonga aliwasilisha salamu za rambirambi kutoka kwa Askofu Jimbo la Kisumu, Kenya Philipo Anyoro na Askofu Jimbo la Malawi, Martin Mtumbuka.

Akitoa salamu za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na za Parokia ya Chuoni hapo, Padri Gallen Mvungi wa Parokia ya Kichangani, alisema ni familia ambayo ilionja upendo wake kwa ukaribu zaidi ambao ulikuwa ukitoka katika nafsi yake.

"Parokia na Chuo tulipata bahati ya kuongea na kushirikishana mengi ya huduma mbalimbali alizokuwa akizitoka, tunawiwa shukrani kwa Mungu kwa maisha na uhai aliomjalia takriban nusu ya maisha yake amehudumia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Mwaka 2022 angeadhimisha jubilei ya miaka 25 ya huduma Chuo Kikuu, kumbe huenda wapo waliopokea upendo huu kwa namna ya kipekee katika miaka 24 ya kuhudumu ambayo si haba," alisema.

Alisema mwaka 2017 alijipatia mtoto ambaye ni Parokia ya Utatu Mtakatifu Changanyikeni.

Mazishi hayo yalihudhuriwa pia na Askofu Mkuu mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Polycarp Kardinali Pengo.

# CTI yakunwa na Rais kuhusu viwanda

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda (CTI), limepongeza hatua zinazochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika maendeleo ya viwanda na kuahidi kushirikiana naye kukuza sekta hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodgar Tenga, alisema hotuba yake ya juzi kuhusu wafanyabiashara itakuza biashara na imani kwa watu wanaotaka kuanzisha biashara.

Alisema CTI imewahi kufanyakazi na Rais wa sasa na inafahamu umahiri wake katika kufuatilia mambo hivyo wenye viwanda wana imani kubwa kwake kwa sababu si mgeni kwao.

"Sisi Rais Samia si mgeni kwetu, tunafahamu uchapakazi wake, hivyo hakuna mwenye kiwanda ambaye shaka na uwezo wake wa kuleta maendeleo. Sisi tunaona ameanza vizuri kwa sababu hababaiki na amenyoosha mambo, tunaomba tumpe ushirikiano mkubwa," alisema.

Tenga alisema tangu aingie madarakani, matamshi yake yamekuwa faraja kwa Watanzania wengi na kwamba hata wafanyabiashara ambao wamekuwa wakimsikiliza wamekuwa wakipata matumaini makubwa kwake.

Alisema wenye viwanda wanajua wajibu wao na CTI imekuwa ikiwasisitiza kufuata sheria za nchi na maadili ya biashara yao ikiwamo kulipa kodi sahihi na kwa wakati.

Tenga alisema CTI imekuwa ikikaa na serikali kujadiliana kuhusu utaratibu rahisi wa kutoa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wageni hivyo hatua ya Rais kukemea urasimu uliopo kwenye vibali hivyo ni ya kupongeza.

katika hatua nyingine, Tenga alisema shirikisho hilo litamuenzi aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli, kwa namna alivyofanikiwa kujenga miundombinu kama barabara, madaraja na ununuzi wa ndege.

"Tutamuenzi Rais wa awamu ya tano kwa mambo mazuri aliyoifanyia nchi hii, wote ni mashahidi kwa namna alivyosimama imara na kufanya mambo makubwa ndani ya muda mfupi wa miaka mitano tu," alisema.

# Maadhimisho ya Miaka 20 Tangu SBC Tanzania Limited ilipoanzishwa

Wiki hii kampuni ya SBC Tanzania Ltd, Watengenezaji na wasambazaji wa vinywaji baridi vinavyopendwa na kuheshimiwa sana Duniani, vya jamii ya Pepsi, Mirinda, Seven Up, Evervess na Mountain Dew.

Inasherehekea kutimiza miaka 20 ya kufanya biashara nchini Tanzania, toka ilipoanza shughuli zake tarehe 05 April 2001.

Tangu ilipoanzishwa, kampuni ya SBC Tanzania Ltd ilikua na Maono ya kutambulika kuwa moja kati ya Makampuni yanayoheshimika sana hapa Tanzania na hivi sasa kwa hakika imeyafikia Maono hayo,

SBC imekua kwa kasi sana na mafanikio haya makubwa yamepatikana kwa sababu ya Wanahisa kuendelea kuunga mkono juhudi za kampuni kwa kuwekeza zaidi bila kuchoka kila kunapohitajika kufanya hivyo.

Kampuni ya SBC Tanzania ina Viwanda vinne hapa Tanzania, ambavyo vipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, na Arusha zikiwemo Depots katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Kilimanjaro. Kampuni imetoa ajira takriban ya watu 3,000 hapa nchini Tanzania na pia imetoa fursa ya biashara kwa maelfu ya Watanzania wanaonufaika kwa kufanya biashara na kampuni ya SBC Tanzania Ltd.

SBC Tanzania inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wafanyakazi wake ambao ndio nguzo na chachu ya mafanikio, bila kuwasahau watoa huduma (Suppliers), Wateja, Washika dau na Washirika wakubwa wa kibiashara, ambao bila ya wao isingekua rahisi kupata mafanikio haya yaliyopatikana.

Kwa kutambua mchango mkubwa wa kizalendo na mfano wa kuigwa wa wananchi, Kampuni ya SBC Tanzania Limited inawashukuru wapendwa Watanzania "Mara Ishirini" kwa kuwapa fursa ya kuchangia na kuongeza thamani kubwa katika uchumi wa Tanzania kwa kutoa fursa nyingi za ajira hapa nchini na wanajivunia kua miongoni mwa Makampuni yanayojulikana kama Walipa kodi wakubwa Tanzania.

Kampuni ya SBC Tanzania Ltd itendelea kuburudisha Taifa la Tanzania kwa kuendelea kuwapatia walaji bidhaa zenye kiwango na ubora wa hali ya juu, kwa bei nafuu kwa miaka mingi inayokuja kwa sababu inaamini kuwa hi ni haki na chaguo lao.Pia SBC Tanzania Ltd itendelea kurejesha kwa jamii kwa kutoa misaada mbalimbali kutoka kwenye Faida inayopata.

Pamoja na hayo itendelea kuhakikisha kuwa kanuni na njia bora zinatumika katika Viwanda vyao ili kuhifadhi maliasili za nchi na kulinda Mazingira

**Mungu Ibariki SBC Tanzania, Mungu Ibariki Tanzania na watu wake, Mungu Ibariki Afrika.**














## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mifuko iwalipe mafao wastaafu kwa wakati

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan, aliwafumbua macho Watanzania juu ya ya kifedha ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kuwa ni mbaya na ndiyo sababu hajateua Mkurugenzi Mkuu.

Aidha, alibainisha kuna kazi ya kufanya ili kuunusuru mfuko huo ili kujua nini la kufanya.

Hadi mwaka 2018 Tanzania ilikuwa na mifuko ya hifadhi ya jamii mitano Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa ajili ya watumishi wa sekta binafsi, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF), Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Akiba wa Watumishi wa Serikali za Mitaa (LAPF) na Mfuko wa Mafao ya Kustaafu (GEPF).

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa umma namba 2 iliyopitishwa na Bunge Januari 31 mwaka 2018 iliunganisha mifuko ya PPF, PSPF, LAPF na GEPF, kuunda mfuko wa PSSSF ambao unawajibu wa kuhudumia watumishi wa umma.

Sheria mpya ndiyo ilileta kikokotoo kipya ambacho kilitaka mstaafu kulipwa malipo ya mkupuo ya asilimia 25, huku asilimia 75 akilipwa kidogo kidogo, utekelezaji ambao kabla ulikuwa uko NSSF, huku mifuko mingine ikiwamo PSPF wakilipa asilimia 50.

Tunakumbuka aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), Dk. Irene Isaka, alivyokaririwa kuwa iwapo utaendelea utaratibu wa zamani, upo uwezekano wa PSPF kushindwa kujiendesha na kulipa wastaafu wake.

Tunafahamu kuwa hifadhi ya jamii ni muhimu sana, kwa kuwa ndiyo maisha ya baadaye ya wastaafu wengi, kwamba wamekatwa fedha zao na kama walikidhi vigezo vya kuchangia michango 180 kwa miaka 15, mfululizo wanastahili ya kulipwa mafao.

Mifuko hiyo baada ya kuunganishwa ilikuja na mafao mapya kutoka kwenye ile ya awali iliyokuwa ina mafao saba ambao ni pensheni ya uzeeni, fao la ulemavu, fao la walithi, fao la upotevu wa ajira, fao la ugonjwa, fao la uzazi na mkopo wa nyumba.

Yote haya ni namna ya kumfanya mstaafu aendelee kuishi maisha mazuri baada ya kumaliza utumishi wake, lakini kama mfuko unakuwa taabani maana yake kuna shida ambayo ni lazima hatua zichukuliwe. Mbali na baada ya kustaafu hata mafao muhimu kama ya uzazi na mengine mtu hatayapata licha ya kila mwezi kukatwa fedha kwa mujibu wa sheria.

Kwa muda mrefu, kuna kilio cha wastaafu wengi wa kwa mujibu wa sheria yaani waliostaafu kwa hiyari kwa umri wa miaka 55 na wa lazima wa miaka 60, kunyimwa au kuzungushwa kulipwa mafao yao kwa sababu ambazo hazijawekwa hadharani kwa usahihi.

Aidha, kumekuwa na ucheleweshaji na uhakiki wa mara kwa mara wa wastaafu ambao wakati mwingine umekuwa ni usumbufu kwa wastaafu kusafiri umbali mrefu, huku wengi wakiwa ni wazee wanaojiuguza maradhi mbalimbali.

Hakuna ubishi kuwa kila mmoja ni mstaafu mtarajiwa, hivyo ni lazima stahiki za wastaafu zinatuzwa vizuri na siyo fedha kutumika kinyume na inapofika wakati wa kulipa inashindikana na wengi kutaabika. Mathalani, mtu anapostaafu anatarajia ndani ya miezi mitatu awe amelipwa haki yake, lakini kwa sasa wapo wanaomaliza mwaka mzima bila kulipwa, huku wengine wakikimbilia kwenye vyobo vya habari.


Mbaya zaidi ni wale ambao hawakutimiza umri wa kulipwa mafao yaani nikuchangia mfululizo miezi 180 na sasa wanatakiwa kulipa michango yao walioyokuwa wamechangia kwenye mfuko, nao kumekuwa na shida kubwa ya kuwalipwa.

Tunaiomba serikali kulitizama suala hili kwa jicho la pekee kuhakikisha wastaafu wanaostaafu kila mwaka wanapata malipo ya mkupuo pamoja na ya kila mwezi kwa mujibu wa sheria, ili kuwa na ustaafu wenye hadhi na siyo kuhangaika wakati fedha zake zilikuwa zinakatwa kila mwezi kwenda kwenye mfuko husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hayati Karume akumbukwa kwa orodha ya mema kwa Taifa

Na Maulid Mmbaga

**KILA** ifikapo April 7, siku kama ya jana, Watanzania wanaadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Zanzibar. Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, aliyezaliwa mwaka 1905 na kufariki mwaka 1972.

Rais Sheikh Karume, aliongoza nchi baada ya mapinduzi yaliyomwangusha Sultani aliyekuwa akitawala Zanzibar, hadi mwaka 1964.

Baada ya miezi mitatu tu, Zanzibar iliungana na Tanganyika ilipokuwa ikiongozwa na aliyekuwa Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Julius Nyerere na kufanya Muungano wa nchi hizo mbili, kukazaa taifa la Tanzania.

Katika maadhimisho hayo, Wazanzibari pamoja na jamii ya Wtanzania kwa ujumla, wanatakiwa kuitumia siku kama ya jana, kutafakari mambo muhimu yatakayoleta mshikamano katika Muungano na yatakayoleta maendeleo ya pande zote mbili.

Watanzania wanapaswa kuulinda na kuuenzi Muungano huo ulioasisiwa uendelee kuleta umoja na ushirikiano katika kutekeleza mambo mbalimbali ya maendeleo yatakayokuza uchumi wa taifa kwa ujumla.

Kwa mwaka huu uliopo ni mara ya kwanza taifa kuidhinisha siku hiyo chini ya marais wapya, Hussein Ali Mwinyi Zanzibar na Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano, ambaye

Ameingia katika wadhifa huo kikatiba, baada ya kufariki kwa aliyekuwa Rais, Dk. John Magufuli.

Sasa kilichopo mbele ya jamii ni kwamba, kila Mtanzania anapaswa kuenzi na kuulinda Muungano wenyewe usitetereke, kwa manufaa ya taifa kwa jumla, kama ambavyo viongozi wakuu wa nchi wanavyosisitiza umuhumu huo.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, juzi wakati alipozungumza katika hafla ya kuapisha makatibu wakuu, manaibu wao na wakuu wa taasisi za umma kadhaa, pamoja na viongozi mbalimbali wa umma alisisitiza haja ya ulinzi wa Muungano.

**Watanzania wanapaswa kuulinda na kuuenzi Muungano huo ulioasisiwa uendelee kuleta umoja na ushirikiano katika kutekeleza mambo mbalimbali ya maendeleo yatakayokuza uchumi wa taifa kwa ujumla.**

Dk. Mpango aliwataka wanaosimamia shughuli za muungano waweze kusimamia ipasavyo wakishirikiana pande zote mbili, ili kupunguza au kumaliza kabisa changamoto zinazotokeza.

"Wale wote wanaoshughulika na Muungano muhakikishe kwamba tunapiga hatua kubwa zaidi ya hapa tulipofika kwa manufaa ya taifa letu," anasema.

Kimsingi, Ofisi ya Makamu wa Rais ndio inawajibika na maendeleo ya Muungano huo na miongoni mwa ufafanuzi katika mustakabali huo, umejumuisha ushirikiano wa kibiashara na miradi ya mkakati na kimaendeleo, itakayobaki kuwa sehemu ya nguzo itakayoendelea kuimarisha mshikamano kwa Watanzania kwa faida ya Taifa kwa ujumla.

Siku hiyo itumike kutafakari mambo mbalimbali ya kimkakati yatakayoisaidia nchi kupiga hatua kimaendeleo, kutoka hapo ilipo aidha kwa kubuni miradi na njia mbalimbali zitakazotupeleka mbele kiuchumi.

Hayati Sheikh Karume, alikuwa miongoni mwa waasisi watakaokumbukwa, si tu kwa historia ya kuongoza nchi pekee, bali inajumuisha mambo mbalimbali aliyolifanyia taifa lake, ambayo bado yadamu kubeba haiba ya faida.

Hapo kunatajwa mengi ya msimamo wa taifa na hadi sasa ikiwamo kushiriki katika suala la kuasisi Muungano

Kila Mtanzania awajibike kuyakumbuka na kuyaenzi mambo ya msingi yaliyokuwa yanasisitizwa na waasisi wa taifa katika kujenga na kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Visiwani kwa faida ya taifa kwa ujumla.

HABARI PICHANI

# RAIS SAMIA SULUHU HASSAN ASHIRIKI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA KARUME ZANZIBAR



Rais, Samia Suluhu Hassan, akiweka shada la maua katika kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, baada ya dua iliyofanyika katika Ofisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kisiwandui Zanzibar jana, katika maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Karume (Karume Day).



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiweka shada la maua katika kaburi la Hayati Abeid Amani Karume.



Mwakilishi wa familia ya Hayati Abeid Amani Karume, Balozi Ali Karume, akiweka shada la maua.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (wa pili kulia), Mjane wa Hayati Abeid Amani Karume, Mama Fatma Karume (wa tatu kulia), Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said (kulia), wakishiriki tukio hilo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, Rais mstaafu wa Zanzibar, Alhajj Dk. Amani Karume, Makamu wa Rais mstaafu wa Tanzania, Alhajj Dk. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Pili wa Rais mstaafu Alhajj Balozi Seif Ali Iddi na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, wakiitikia dua wakati wa kisomo cha hitma na dua ya Hayati Abeid Amani Karume.



Viongozi wa dini na waumini wa Kiislam wakisoma hitma na dua kumuombea Hayati Abeid Amani Karume. **PICHA ZOTE: IKULU**

# Mwisho katazo mifuko ya plastiki leo

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema leo ni mwisho wa matumizi ya mifuko ya plasitiki, ambayo haikidhi vigezo pamoja na kuthibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Aprili 5, mwaka huu NEMC iliwakumbusha watumiaji wa mifuko ya plastiki kwamba, mwisho wa matumizi hayo ni Aprili 8, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka lipozungumza Nipashe, alisema kama ilivyotangazwa awali na baraza hilo, kuhusu ukomo wa matumizi ya mifuki hiyo, ni vyema jamii ikaanza kutumia vifungashio mbadala.

Mapema, Machi mwaka huu, Dk. Gwamaka akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, alisema hakutaongezwa muda wa kusitisha matumizi ya mifuko hiyo kutokana na awali kuchukuliwa hatua kama hiyo.

Dk. Gwamaka alibainisha kwamba, kwa ambao watakiuka katazo la matumizi ya mifuko hiyo, adhabu yake ni pamoja na faini ya kuanzia Sh. 30,000 hadi 200,000 kutegemeana na kosa.

Pia, alisema kuwa wazalishaji wakubwa wa bidhaa za vifungashio vya plastiki ikiwamo viwanda adhabu ni faini ya Sh. milioni tano hadi Sh. bilioni 10 kutegemeana na aina au ukubwa wa kosa.

"Desemba 31, mwaka jana, NEMC, tulkumbusha kuhusu kanuni kwamba ilisemavifungashio ambavyo havijakidhi vigezo visionekane katika mazingira. Ili kwa wanaotumia vifungashio na kutengeneza kwa wingi wasajiliwe au kupewa maelekezo," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema lengo la kanuni na katazo hilo ni kulinda mazingira na kuwa endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Dk. Gwamaka alisema kanuni iliwekwa ili kulinda mazingira, kupunguza uchafuzi kutokana na mifuko ya plastiki ambayo haiwezi kurejelezwa ambayo haiozi isiyooza ardhini kwa takribani miaka 400 hadi 500.

"Tusiishi kama sisi ndio kizazi cha mwisho katika hii dunia, kwa kuchafua mazingira kana kwamba hakuna viumbe wengine baada ya kizazi hiki, tumeikuta ardhi safi na sisi tunaiacha chafu, si sahihi," alisema Dk. Gwamaka. Alisema wanaozalisha vifungashio wana wajibu wa kuzirejesha bidhaa zao viwandani ili kulinda mazingira na kwamba wajasiriamali na wafanyabiashara wageukie matumizi ya mifuko ya karatasi na katani kwa kuwa kuna viwanda vinavyozalisha nchini.

"Tarehe 8 , Januari mwaka huu, waziri wa nchi ofisi ya makamu wa rais, alionyesha huruma na kuongeza muda wa matumizi ya mifuko hii, sheria inakataza ndio maana wakapewa miezi mitatu, kusiwe na bidhaa ambayo TBS (Shirika la Viwango Tanzania) haijaruhusu, haijasiliwa na kuwa sokoni.

Kadhalika, Dk. Gwamaka aliwataka wenye viwanda na wajasirimali wa bidhaa za vyakula, mifugo na kilimo kuanza kujiandaa kutumia vifungashio mbadala rafiki wa mazingira, ili kuepuka adhabu.

"Muda huo ukifika hatutarajii walio na viwanda kuona kama tunawaonea ndio maana tunaawarifu mwezi mmoja umebaki, matumizi ya mifuko hii, iwe ni wauza miwa, yeyote,

# Rais Samia ahofia kifo cha Ngorongoro

**Na Salome Kitomari**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema bila hatua madhubuti za kuiokoa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), kuna uwezekano mkubwa wa kupotea na kubaki historia.

Samia alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na viongozi mbalimbali wa serikali baada ya kuwaapisha makatibu wakuu, manaibu na wakuu wa taasisi walioteuliwa Aprili 4, mwaka huu, kushika nyadhifa mbalimbali.

"Ngorongoro inapotea, tulikubaliana na eneo la aina yake watu na wanyama wakae pamoja, lakini sasa watu wanazidi kuliko wanyama," alisema.

"Tulipoingia huu mkataba (mkataba wa maisha ya binadamu na wanyama kutumia eneo moja) tulikuwa na watu 9,000 na sasa ni kati ya 90,000 na 100,000, NCAA na Wizara mpo mnawaangalia, maeneo yanachukuliwa mpo.

"Tulikubaliana watu na wanyama wakae pamoja lakini si kwa kiasi hiki, watu 100,000 kwa wanyama wale lazima watazidiwa," aliongeza.

Pia alisema Ngorongoro inatoweka kutokana na uvamizi wa mimea vamizi inayomaliza mimea muhimu kwa ajili ya malisho ya wanyama.

"Kama tunataka Ngorongoro ibakie na inauza Tanzania tuwe makini kuitunza na kuhakikisha inabakia. Kuhamisha watu sijui mtafanyeje, kama wameshaingia 100,000 sijui mtafanyeje.

"Ila cha kushangaza wengine wafanyakazi wa Ngorongoro wanamega maeneo na kuanza kuishi," alisema.

Desemba, mwaka jana, wakati wa Mkutano baina ya NCAA, wahariri na waandishi waandamizi, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Freddy Manongi, alisema kuna umuhimu wa kamisheni ya kuchunguza na kuja na matokeo ya kisayansi juu ya namna ya kulitumia eneo hilo.

Alisema kwa sasa hali ni ngumu kwa uhifadhi kwa kuwa kila hatua inayochukuliwa kwa ajili ya uhifadhi, ina athari kwa wananchi wanaoishi ndani ya eneo hilo na kila shughuli za kibinadamu zinazofanyika zina athari kwa uhifadhi, na kwamba idadi ya watu imeongezeka kutoka 8,000 mwaka 1959 hadi 100,000 kwa sasa.

"Najaribu kuitazama Ngorongoro miaka 10 ijayo kwamba itakuwa katika hali gani kama kasi ya watu itakuwa hii, shughuli za uhifadhi zitakuwa ngumu, migogoro baina ya jamii na wanyama itaongezeka, tutawezaje kwenda pamoja na maendeleo endelevu ya binadamu na uhifadhi," alisema Rais.

KuhusuKamisheniiliyoundwa mwaka 2019, ilihoji watu mbalimbali na ulimaliza kazi Mei mwaka jana, na mapendekezo ya awali ilikuwa ni kuligawa eneo la Ngorongoro kwa kanda kulingana na shughuli zilizopo.

Eneo la Ngorongoro lilianza mwaka 1959 baada ya kumegwa kutoka eneo la Serengeti Game Reserve na kuunda Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliyopo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), kwa watu 4,000 kuhamishiwa ndani ya eneo na kuwa na jumla ya watu 8,000 ambao wameongezeka na sasa ni zaidi ya 100,000.

**MADINI HIFADHINI**

Rais Samia alisema kuna haja ya kuangalia suala la uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya Hifadhi za Taifa zilizo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), huku akitaka wataalam kuangalia suala hilo kwa jicho la pekee.

"Unajua kuna madini katika maeneo yako ya TANAPA na wakati ule uliweka misuli hapa hapachimbiki hapa, hamuingii, lakini uhifadhi tunautaka, madini tunayataka, madini mengine ni muhimu sana kama Helim,"alisema na kuongeza:

"Madini yapo mchimbaji yupo kila siku anagonga mlango kok kok mlango haufunguki, kila akigonga umefungwa, hebu tukaeni tumalize pachimbwe, tunayaweka pale ya nini, simba sijui tembo hali yale, tunayaweka ya nini, ingekuwa wanayala tungesema tunapunguza 'share' (mgawo) ya wanyama wetu, na kama ni kuunguza eneo tuangalie gharama ya kupunguza eneo la hifadhi na gharama ya kuchimba, tumalize haya tusonge mbele."



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa kituo cha mabasi ya mwendokasi lilipokuwa eneo la stendi ya mabasi ya mikoani, Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jafo awapa ujumbe vijana kuuenzi Muungano

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amewataka vijana kuendelea kuuenzi Muungano kwa kudumisha amani.Jafo alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kuhudhuria dua maalum ya kumwombea Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hayati Abeid Aman Karume, iliyofanyika katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui.Alisema vijana wa sasa wanapaswa kuona fahari ya Muungano na kuyaenzi yale yaliyoachwa na Hayati Karume ambaye ameacha alama Zanzibar, hususan katika ujenzi wa miundombinu na kuwajali wananchi.

Jafo alisema kiongozi huyo alikuwa na maono makubwa kwa wananchi wake na kuwa mfano wa kuigwa kwa viongozi wengine nchini na Afrika kwa ujumla.

"Tukumbuke kwamba Hayati Karume na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, walifanya kazi kubwa ya kuasisi Muungano na leo hii tunajivunia kuwa Watanzania, hivyo kwetu sisi ni faraja, hatuna nchi nyingine isipokuwa ni Tanzania," alisema.

Waziri Jafo pia alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, kwa uongozi wake ambao umewafanya wananchi kuwa na imani kubwa kwake.

Alitoa rai kwa Watanzania kumuunga mkono kwa yale anayoendelea kuyatekeleza na kuwa ameonyesha weledi katika utendaji wake ambao unaakisi aliyofanya Hayati Karume, hasa katika ujenzi wa makazi bora kwa wananchi.

Aprili 7 ya kila mwaka ni kumbukumbu ya kifo cha Karume ambaye alifariki dunia mwaka 1972 na Dua Maalum ya kumwombea ilifanyika visiwani hapa jana, ikihudhuriwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na viongozi mbalimbali wa kitaifa.

## Familia maskini zawezeshwa kwa majiko ya gesi

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

TAASISI ya kusaidia watu wanaoishi katika mazingira magumu Tanzania (TAPO), imetoa msaada wa majiko 10 ya gesi kwa familia 10 zinazoishi katika mazingira magumu katika Manispaa ya Morogoro.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano iliyofanyika juzi katika ofisi za taasisi hiyo, mratibu wa TAPO, Anthony Maskati, alisema msaada huo ni kwa ajili ya kuwapatia faraja watu hao wanaoishi katika mazingira magumu hasa kwa kupata lishe bora kama ilivyokatika familia nyingine

Alisema tangu kuanzishwa kwa shirika hilo, zaidi ya watu 500 wameshafikiwa, ambapo kati yao zaidi ya familia 100 zimeshakuwa na uwezo wa kujikimu kimaisha, na kwa kuimarika kiuchumi ambapo kwa sasa wanajitegemea wenyewe.

"Moja ya sera ya taasisi yetu ni kusaidia shughuli za kijamii ikiwamo kuunga mkono jitihada za serikali za kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizopo kwenye jamii, ndio maana leo tumeona kuna umuhimu wa kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika Manispaa ya Morogoro wakiwakilishwa na familia zao," alisema Maskati.

Kadharika, alisema kuwa licha ya kuwasaida watoto wenye mazingira magumu katika misaada hiyo, wamekuwa wakijihusisha na kuwalipia ada za shule watoto hao ili kutimiza ndoto zao.

Akitoa shukrani kwaniaba ya wazazi na watoto hao, Sabra Issa, alisema wanashukuru shirika hilo kwa msaada walioutoa kwa sababu utasaidia kwa kiasi kikubwa kuwapunguzia gharama za maisha tofauti na awali walipokuwa katitumia nishati nyingine kama mkaa na kuni.

Pia, aliomba shirika hilo kuongeza nguvu katika kusaidia elimu kwa watoto hao kwani licha ya kujitolea kuwalipa ada bado, kumekuwapo na kikwazo cha baadhi ya wanafunzi kukatisha masomo yao kwa kisingizio cha ugumu wa maisha na kukimbilia mtaani kujihusisha na ajira zisizo rasmi.

# Wasakwa kwa tuhuma za kutishia viongozi kwa jeneza

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

SERIKALI inawasaka watu wote walioshiriki kubeba jeneza na kwenda kulitelekeza kwenye ofisi za Kijiji na Kata ya Namwinyu wilayani Tunduru Mkoa wa Ruvuma kwa nia wa kuwatishia viongozi wa serikali kuacha kutimiza wajibu wao.

Melezo hayo yametolewa na,Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji hicho, baada ya kujionea tukio hilo ambalo lilisababisha taharuki kwa watumishi na wananchi kijijini hapo.

Aidha kupitia taarifa hiyo, Mtatiro aliwaonya wananchi kuacha vitendo hivyo kwani siyo vya kiungwana, na kwamba vinaonesha jamii hiyo kuendekeza imani na mila potofu za mambo ya kishirikina. Awali Ofisa Tarafa ya Matemanga, Emilias Njogopa, alisema baada ya kupokea taarifa ya kutelekezwa kwa jeneza hilo kutoka kwa watendaji wa kijiji na kata hiyo, alipeleka taarifa hiyo wilayani ili waweze kulitambua tukio hilo.

Alisema taarifa zinaeleza kuwa Jeneza hilo liliwekwa katika ofisi hizo ikiwa ni ishara ya baadhi ya wananchi kutuma ujumbe wa kuwatishia viongozi hao kuacha utekelezaji wa sheria ndogo waliyojiwekea ya kukamata mifugo, ambayo imekuwa iki funguliwa na kuachwa bila uangalizi na kuwatoza faini wamiliki wa mifugo hiyo.

Naye Mwenyekiti wa serikali ya Kijiji cha Namwinyu alisema baada ya tukio hilo, ofisi yake imekaa na wazee maarufu na kutafutia ufumbuzi wa kudumu juu ya matukio ya vitisho vya aina hiyo kwa watumishi wa serikali, ambayo yanaweza kuharibu taswira ya kijiji chao.

Diwani wa Namwinyu, Matumla Said, alisema tukio hilo limewafadhaisha sana viongozi hao kwani wanachokifanya ni utekelezaji tu kwa kuwa sheria hiyo ndogo ilipitishwa kwenye vikao halali na baadae kuwashirikisha wananchi wote kupitia mikutano ya hadhara.

Hili ni tukio la pili katika kipindi cha mwaka huu kwa watumishi kuwekewa majeneza na wananchi kama sehemu ya vitisho dhidi ya watumishi wa serikali, ambapo tukio la kwanza lilitolea Februari 22, mwaka huu ambapo wanachi wa kijiji cha Mfuate Kata ya Likuyu wilayani Namtumbo walitelekeza jeneza nyumbani kwa mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Mfuate.



Mkurugenzi wa kampuni ya Xing J.X ya China, Xheng Jian, akikabidhi msaada wa bidhaa mbalimbali kwa Katibu wa Kituo cha Kulea watoto yatima cha Malaika, Khadija Said, kwa ajili ya matumizi ya watoto wanaolelewa katika kituo hicho, jijini Dar es Salaam, jana. Kushoto ni Mfadhili wa kituo hicho, Juma Gurumo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kanisa lawakumbuka wafungwa, mahabusi

**Na,Said Hamdani,** LIWALE

UONGOZI wa Kanisa la Anglikana Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi wakishirikiana na waumini wao limewafariji wafungwa na mahabusi wa Gereza la Kipule,kwa kuwapatia msaada wa bidhaa mbalimbali.

Baadhi ya vitu hivyo sukari, sabuni, dawa za mbu, miswaki na dawa zake pamoja na nnembe kwa ajili ya usafi wa nywere na mavazi kwa waliopo maabusi, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. 200,000.

Msaada huo ambao ulikabidhiwa kwa uongozi wa gereza hilo na Mchungaji wa Kanisa hilo, Augustino Kinyama, aliyeongozana na baadhi ya waumini.

Mchungaji Kinyama akizungumza na wafungwa na mahabusi, aliwataka kubadilika na kuishi maisha ya usafi na unyenyekevu yanayompendeza Mungu ili kuliwezesha Taifa kuendelea kupata baraka zake.

Alisema msaada walioutoa kwao ni moja ya kuwatia moyo wafungwa na mahabusi waliopo ili watambue kama wapo pamoja nao licha ya kwamba wapo gerezani kwani sio wote waliopo huko wana makosa.

Mchungaji huyo aliwaomba wafungwa na mahabusi waliopo kwenye gereza hilo kuwa watiifu na kutubu makosa wanapokuwa gerezani na watakapokuwa nje uraiani.

Rodrick Kapanda, alilipongeza kanisa hilo kwa msaada huo, kwani umefika kwa wakati mwafaka na kuahidi kufikishwa kwa walengwa, huku akiziomba taasisi zingine kufuata nyayo hizo, kwa ajili ya kuisaidia serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Mmoja wa wafungwa hao akitoa shukrani zao kwa niaba ya wenzake, walilishukuru kanisa hilo kwa msaada waliopatiwa, huku wakiahidi kuwa watiifu na raia wema wawapo gerezani na pale watakapokuwa wamerejea uraiani.

# Faida za kupanda miti asili zaanikwa

**Na Christina Haule,** LINDI

WILAYA ya Lindi imewataka wadau wa misitu kuona umuhimu wa kuilinda na kupanda miti ya asili ikiwamo mininga na mivule ili kufanya miti hiyo kutambulika na vizazi vijavyo na kutobaki kuwa historia.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa mashine ya kuchakata magogo yenye thamani ya Sh. mil 110 iliyotolewa na Programu ya mnyororo wa Thamani wa mazao ya misitu (FORVAC) kwa ufadhili wa Serikali ya Finland na Tanzania itakayotumiwa na wanavijiji 18 wa Wilaya za Nashingwea na Ruangwa mkoani humi.

Ndemanga alisema wilaya ikiwa ndio wadau wakubwa wa misitu imepanda vitalu vyenye miche zaidi ya laki moja ambayo wanajipanga kuigawa kwa wananchi na taasisi.

Alisema wadau wa misitu ikiweko Wakala wa Misitu (TFS) wameanza kuonyesha juhudi za kupanda miche hiyo ili kufanikisha uhifadhi wa miti hiyo ya asili.

Alisema utaratibu huo walianza mwishoni mwa mwaka jana kwa kuanza kupanda kitalu chenye miche zaidi ya 100,000 kwenye eneo la msitu wa Serikali wa Londo ambayo wanategemea kuipanda kwa kushirikiana na jamii wakati wa kipindi cha msimu wa mvua za masika katika maeneo mbalimbali wilayani humo.

Aidha Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wakuu wa shule zote za msingi na sekondari wilayani humo kupanda miti hiyo kwenye mashamba yenye ukubwa wa heka 3 hadi 4 ili kuendeleza uhifadhi wa misitu wilayani humo.

"Upandaji wa miti hii katika maeneo ya shule utawafanya wanafunzi kuitambua na kuona na pengine kujifunza namna ya usimamizi shirikishi wa misitu unavyokuwa," alisema.

Alisema kwa kushirikiana TFS wameona umuhimu wa kupanda miti yote ya asili ambayo ipo hatarini kutoweka ambayo ni pamoja na mipingo, mivule, mikongo, misekeseke na mininga.

Naye Kamishna Msaidizi kutoka TFS Kanda ya Kusini, Manyisye Mpokigwa, alisema katika kutekeleza mpango wa upandaji miti ya asili wilayani humo, kanda hiyo.Katika mwaka wa fedha 2020/21 walifanikiwa kupanda miche mil 3 ili kurudisha uoto wa asili.



Wanakijiji wa Kijiji cha Pwaga, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma, wakichota maji katika moja ya kisima kijijini hapo juzi, ambapo mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF), umewawezesha fedha na kwa ajili ya kuchimba bwawa la maji. PICHA RENATHA MSUNGU

# Wanufaika TASAF waongeza uzalishaji kilimo

**Na Elisante John,** SINGIDA

WANUFAIKA wa mfuko wa maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) katika Wilaya ya Iramba mkoani Singida, wameanza kujikomboa kiuchumi kwa njia ya kilimo, baada ya kuongeza uzalishaji shambani.

Wameongeza uzalishaji kutoka gunia moja hadi 15 kwa ekari moja, kwa fedha za ruzuku inayotolewa na serikali.

Hayo yalibainishwa na walengwa wa TASAF, baada ya kutembelewa na maofisa wa TASAF kutoka makao makuu jijini Dodoma na waandishi wa habari, juu ya mafanikio waliyopata kupitia miradi waliyoanzisha ili kujikomboa kiuchumi kwa fedha za ruzuku.

Akizungumzia maendeleo hayo, mkazi wa Kitongoji cha Mang'ata katika Kijiji cha Old Kiomboi, Marian Msengi (59), alisema kuwa ongezeko la mazao hayo limetokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na TASAF, ikiwamo kupatiwa wataalamu wa ugani kwa ajili ya kuwapatia mbinu za kilimo chenye tija.

"Wataalamu wa kilimo wamenisaidia sana katika kilimo kupitia ruzuku ya Sh. 62,000 ninayoipata...zamani nilikuwa navuna madebe matano tu, lakini mwaka jana nimeongeza mpaka magunia 15 kwa ekari moja," alisema Mariam.

Naye Neema Shani (25) wa Kitongoji cha Nsuile katika kijiji hicho, alibainisha kuwa kupitia mradi wa wasichana balehe walio ndani na nje ya shule, kwa kushirikiana na mama yake, ameongeza mavuno shambani hadi kufikia magunia sita kutoka moja la awali, huku pia akifanikiwa kuanzisha mradi wa ufugaji ambapo hadi sasa ana jumla ya kuku 42 wa kienyeji, huku wengine wa awamu ya kwanza akiwauza na kujipatia kipato cha zaidi ya Sh.200,000.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Iramba, Adam Msangi, alisema hadi sasa zaidi ya Sh. bilioni 7.9 zimetumika kwa walengwa 5,206, tangu mradi wa kunusuru kaya masikini uanze aprili 2014 kwa vijiji 51 kati ya 70 vya wilaya hiyo.

Kwa mujibu wa ofisa uhusiano wa TASAF, Estom Sanga, idadi kubwa ya walengwa wa kunusuru kaya zilizo masikini zaidi zimejipatia maendeleo, hivyo hashangai kuona idadi kubwa ya walengwa ikiongeza uzalishaji wa mazao, kupitia kilimo.

# Zahanati ya polisi ilivyoondoa adha ya msongamano

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

ZAHANATI ya kituo cha Polisi wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imesaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa wanaofika katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Mjini kupata huduma za matibabu ukilinganisha na awali ilivyokuwa.

Hospitali hiyo kwa siku inahudumia wagonjwa 1,000 hadi 12,00 kutoka Halmashauri za Msalala, Ushetu, Kahama Mjini, Shinyanga Vijijini, Mbogwe, Masumbwe, Kakonko, Kibondo na baadhi ya wilaya zilizopo mkoani Tabora na kusababisha kuwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa.

Hata hivyo ili kuendelea kupunguza wimbi la wagonjwa katika Hospitali hiyo, Halmashauri hiyo ilitenga cha Sh. bilioni 3.2 za mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kupumzikia wagonjwa wa nje lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini.

Marki Juma, Ofisa tabibu wa zahanati hiyo, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili ofisini kwake, akitoa taarifa ya huduma zinazotolewa na zahanati hiyo ikiwamo huduma ya mama na mtoto, maabara, uzazi wa mpango na kliniki kwa watoto wadogo chini ya miaka mitano.

Alisema mwezi uliopita walitoa huduma kwa wagonjwa zaidi ya 660, wajawazito wakiwa 43, chanjo kwa watoto wadogo 437, uzazi wa mpango 24 na wagonjwa wa nje wakiwa 155 na asilimia kubwa ya wagonjwa wanatoka Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Alisema wagonjwa wengi wanafika katika zahanati hiyo kupata huduma, wanaepuka msongamano wa wagonja katika hospitali ya wilaya, hasa wakati wa kliniki kwa watoto wadogo ambapo wengi wao huamka alifajiri na kuja kupata matibabu saa nne asubuhi.

Nae Lidia Saguda, mmoja wa kinamama aliyefika zahanati kupata huduma, alisema wanafika katika zahanati hiyo kupata huduma kwa kuepuka msongamano wakati wa kiliniki katika Hospitali ya Wilaya, nakwamba unaweza kuamka saa 12 alfajiri na kuja kuapata huduma saa tano asubuhi.

"Ukweli zahanati hii imepunguza msongamano wa wagonjwa, tulikuwa tunaamka alfajiri na kupata huduma saa nne asubuhi na wakati mwingine mchana....sasa tunapata huduma kwa wakati na kupata muda wa kufanyakazi za kujenga Taifa tofauti na awali," alisema Saguda.

Nae Samweli Alphance, alisema kila siku za kliniki kwa ajili ya mtoto wake, amekuwa akienda na mkewe, na kwamba wanapata huduma kwa haraka ukilinganisha na wale wanaokwenda wenyewe bila waume zao.

ama
ALHAMISI APRILI 8, 2021
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 14



**Kwanini vidonge vya uzazi vya kinababa ibaki bidhaa adimu ?**



Ukurasa 13

Wakazi Babati katika tabasamu mradi maji tangu kupata uhuru




Ukurasa 12

**UBUNIFU MPYA DUNIANI...**

**Mabinti watano shuleni walivyoibua kifaa kinachodhibiti mbu wa malaria**

# Kiama cha mwezi mmoja ujao dhidi ya maabara bubu mitaani

- Holela uchochoroni 'hatari tupu watoto'

**Na Yasmine Protace**

PANAPOKUWAPO maabara sehemu yoyote, huwa kuna maana ya kuwahudumia wananchi wa hapo au kutoka maeneo mengine.

Maabara zimekuwa msaada tosha na kimbilio pale ambapo mtu anakwenda kwa ajili ya kupata huduma za kiafya.

Zipo maabara ndani ya zahanati, vituo vya afya na hospitali na zingine ambazo hazipo huko, ziko huru zinajitegemea.

Mkurugenzi wa Huduma na Tiba kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Magembe, sasa anazitaka maabara zilizojengwa katika makazi ya watu, kuwa na tahadhari ya kiafya, kwa jamii zinazozizunguka.

Anasema, serikali inazitaka kuwaangalia kwa karibu jamii jirani na na hasa watoto, kwani wanaweza kuchezea taka hatarishii, sambamba na wanajamii, kuwa makini na watoto wanaoweza kuchezea taka kujikuta wanakumbwa na magonjwa makubwa.

Kiongozi huyo anasema hadi sasa kuna kila sababu ya jamii kuwa makini na michezo ya watoto wanaocheza jirani na maabara, akitaja maabara kuna vipimo vingi vinavyochukuliwa kwa wagonjwa na taka zisipohifadhiwa vizuri, watoto wanaweza kupata magonjwa.

Hivyo anasema, maabara zinatakiwa kuwa katika maeneo ambayo hayataleta changamoto kwa wananchi wanaozunguka katika maeneo hayo.

Tahadhari yake ni kwamba maabara zinapofunguliwa katika makazi ya watu, ziko katika hatari ya kueneza madhara kwa watoto, kwani wanapenda kuchezea vihatarishi vya afya.

Kwa mujibu wa Dk. Grace, nia mojawapo bora ya kujihami na hatari hiyo ni maabara kujengwa mbali na makazi ya watu, kwani ujenzi au uzalishaji maabara mitaani, ni hatari iliyo jirani na umma.

**MAABARA BUBU**

Pia, Mkurugenzi ana dhamira ya pili, katika haya ya kupambana na maabara bubu, zinazotoa huduma na hatia ya sasa, serikali imezitaka hadi kufikia mwisho wa mwezi huu tarehe 30, ziwe zimesajiliwa na kama zitakuwa hazijasajiliwa, hatua kali dhidi ya wamiliki zitachukuliwa.

Dk, Grace akizungumza katika mkutano na wamilikiwa maabara binafsi za Mkoa wa Dar es Salaam, anawataka wamiliki wa maabara bubu nchini ambazo hazijasajiliwa, wamepewa kipindi cha mwezi mmoja Aprili 30 wawe wamesajili ili kuepuka kufungiwa.

"Kumekuwapo maabara mitaani ambazo hazijasajiliwa na zinaendekeza kutoa huduma. Kinachotakiwa ni kuzisajili mpaka mwishoni mwa mwezi huu.

"Nimetoa maelekezo kwa Mratibu wa Maabara Mkoa wa Dar Es Salaam, kuhakikisha maabara zote ambazo hazijasajiliwa zipewe nafasi ya kusajiliwa hadi kufikia tarehe 30 mwezi Aprili.

"Kinyume na hapo zitafungiwa na wahusika kuchukuliwa hatua kwa kupelekwa kwenye vyombo vya sheria," anaagiza mkurugenzi huyo.

Dk. Grace, pia anakumbusha huduma za maabara kuwa nyeti na zinazohusika moja kwa moja na afya ya mwanadamu, hivyo pale zinapotoa majibu yasiyo sahihi, zinaweza kuhatarisha maisha ikiwa hatua stahiki hazitachukuliwa.

Mkurugenzi huyo anasema hadi sasa kuna baadhi ya maabara zisizo na wataalamu wenye vigezo vinavyotakiwa au kuwa na upungufu kulingana na kazi zilizopo.

Kutokana na uhalali huo, pia ameziagiza ndani ya mwezi mmoja unaotimu Aprili 30, wamiliki wa maabara hizo wawe wameshapata wataalamu wanaostahili kuwafanyia kazi hizo.

Dk. Grace anawataka viongozi wa ngazi mbalimbali za mitaa, vijiji na vitongoji kutoa taarifa kwenye mamlaka husika, endapo wataona kuna maabara zimeanzishwa katika maeneo yao ambazo hazijasajiliwa.

Msajili wa Maabara Binafsi, Dominic John, amesema lengo la mkutano huo ni kuwaleta wataalamu na wamiliki wa maabara wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja, ili waweze kupata miongozo na namna ya kuendesha maabara zao kwa usahihi na kutoa huduma bora kwa wananchi.



Mkurugenzi wa Huduma za Tiba katika Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Grace Magembe, akiongea na wamiliki wa maabara (hawapo pichani). **PICHA: YASMINE PROTACE**

AFYA

UBUNIFU MPYA DUNIANI...

# Mabinti watano shuleni walivyoibua kifaa kinachodhibiti mbu wa malaria

- Ngurumo aina yake inayomfukuza
- Watua vyuo vikuu, yumo wa udaktari

**Na Christina Mwakangale**

MTU anapozungumzia kuwapo ugonjwa wa malaria, katika nchi zinazoendelea utabaini ni kati ya vinavyosababisha kurudisha maendeleo nyuma.

Kwa maana malaria huathiri zaidi mataifa ya Kusini mwa Jangwa Sahara, katika baadhi ya mataifa ya Asia na Amerika ya Kusini, ambayo ugonjwa huo una tiba, licha kusababisha vifo vingi duniani.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema kuna kifo cha mtoto mmoja kila baada ya dakika mbili, huku ongezeko jipya la wagonjwa zaidi ya milioni 200 wakiripotiwa kila mwaka.

Jukumu la kukabiliana na ugonjwa huo linaendelea kutafutiwa ufumbuzi na wataalamu wa afya, huku WHO ikipendekeza walio katika hatari ya kupata malaria wakingwe kwa kutumia mbinu zilizothibitishwa kuwa bora zaidi.

Hapo zinatajwa mbinu kama matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa (ITN) na kupulizwa dawa ndani na nje ya nyumba (IRS).

### WABUNIFU WAJITOKEZA

Katika kuongeza juhudi za kupambana na ugonjwa huo, wapo wanasayansi wanaochipukia, wasichana watano wahitimu wa Shule ya Sekondari Jangwani, wamebuni mbinu mpya ya kujikinga malaria, wakiitaja kuwa rafiki wa mazingira.

Paulina Haule, mmoja wa wabunifu hao wa kifaa hicho kiitwacho 'Ultraltraconic Mosquito Repellent' anasema wazo la ubunifu wao, umeboreshwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kupitia Atamizi ya Teknohama ya Dar es Salaam (DTBi).

Kupitia ubunifu huo mwaka 2019, Paulina pamoja na wenzake wane; Grace Yusto, Julieth Maisorry, Bupe Mayala na Nia Mfaume, walitunukiwa tuzo iitwayo 'Project Pitching Winners 2019' iliyotolewa na mradi wa Future STEM Business Leaders (FSBL).

Mpango huo huwaendeleza kwa kuwapa ujuzi wanafunzi wa masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kutoka katika shule mbalimbali ambao ulioanza mwaka 2017.

Akizungumza na hivi karibuni kwa niaba ya wenzake Nipashe, Paulina anasema, mradi huo umekuwa mpya na kugundua mambo kadhaa maishani.

"Nimekuwa mtu mpya kabisa na nimegundua kwenye maisha yetu kuna matatizo ambayo ni mengi tunaweza kuyatatua, licha tu ya kuwa na elimu ya darasani.



Paulina alipofafanua kuhusu hali ya mradi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

> **Watu huchukulia sayansi ni somo la jinsia, gumu labda watoto wa kike hawawezi wakalimudu, kila mmoja anaweza akalisoma akitulia.**

"Elimu ya darasani tunaweza kuibadili kuwa halisi hata katika biashara na kufanya mambo mengi katika maisha yetu ya kawaida. Natamani wanafunzi wanaokuja wajue namna ya kutumia elimu ya darasani," anasema Paulina.

Paulina anasema, amehitimu masomo ya kidato cha sita katika Shule ya Sekodari Jangwani mwaka, jana na sasa anasoma Shahada ya kwanza katika chuo cha St. Joseph akiwa katika taaluma ya utabibu.

"Watu huchukulia sayansi ni somo la jinsia, gumu labda watoto wa kike hawawezi wakalimudu, kila mmoja anaweza akalisoma akitulia.

"Ni 'exposure' (uelewa) kupitia mradi huu na nimepata mwamko mkubwa wa kusimama mbele za watu. Kwanza, ifahamike kisayansi mazingira yetu mbu ni muhimu na hawatakiwi kufa katika mazingira yetu, sababu kuna viumbe wanawategemea, hivyo kifaa hiki kinafukuza mbu na si kuua," anasema.

Anasema, kifaa hicho kinatumia sauti zenye mlio wa chini ambao binadamu hausikii ila mbu pekee na kwamba mbu akizisikia sauti hizo huhisi usumbufu na kukimbia.

"Kifaa kinatumia frequency (mzunguko) wa mawimbi sauti yenye mlio mdogo ambao unampiga mbu na kumfanya akimbie asikae eneo hilo.

"Sauti hizo binadamu huwezi kuzisikia, lakini kwa mbu kwake ni sauti kubwa mno. Kifaa hicho ni rafiki wa mazingira hakitoi harufu hakina kelele na kinabebeka. Tulipogundua kifaa hiki ukikiona kina muonekano mkubwa, lakini kikiendelea kuboreshwa kitapungua," anasema.

Paulina anabainisha kwamba, kwa sasa hakuna teknolojia kama hiyo popote duniani, huku wakisubiri kukamilisha usajili na kupata haki miliki.

"Tunasubiri tukamilishe kila kitu ili tupate haki miliki na kuingia sokoni. Tunashukuru programu hii ya FSBL kuibua huu ubunifu. Kifaa kina uwezo kutumia umeme wa jua au umeme wa kawaida," anaeleza Paulina.

Paulina anakamilisha kwa kusema mradi huo umemjengea ujasiri wa kuongea na ilikuwa si rahisi kujinadi mbele ya watu, sasa amebadilika.

### WADAU COSTECH

Mkurugenzi Mkuu COSTECH, Dk. Amos Nungu, akizindua rasmi mradi wa Future STEM Business Leaders (FSBL) kupitia Atamizi ya Teknohama ya Dar es Salaam (DTBi), wiki hii jijini, anasema mradi huo ulianza mwaka 2017 kupitia DTBI.

Hadi sasa anaeleza kuwa ana uzoefu wa kuwajengea uwezo vijana kubuni na kukua kibiashara, unafanyika kwenye shule 13, kati yake nane kutoka Dar es Salaam na tano Arusha.

Dk. Nungu anasema, ni mradi utakaowajengea uwezo wanafunzi hao katika kupitia masomo ya sayansi na kubaini fursa za kujiajiri na kuajiri.

"Wadau wa elimu na jamii iwaandae vijana ili kuitumia elimu wanayoipata shuleni hususan somo la sayansi, kutatua matatizo kwenye jamii," anasema Dk. Nungu.

Anasema kutokana na dunia kukua kidigitali, ipo haja ya wanafunzi kuandaliwa tangu sekondari badala ya kusubiri wafike ngazi ya juu kama chuo kikuu.

"Mradi unasimamiwa na COSTECH kupitia DTBi, umefadhiliwa na Idara ya Fizikia ya nchini Uingereza. Unatekelezwa pia tukishirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Fizikia na Arusha Tech," anasema Dk. Nungu.

Kadhalika, Dk. Nungu anatoa wito kwa vijana kuwa sehemu ya utatuzi wa matatizo yaliyopo kwenye jamii kwa kutumia teknolojia.

"Msiikimbie sayansi! Vijana wengi wanakuja na mawazo yenye ubunifu lakini hayafanyiwi kazi, kupitia mradi huu wataibuliwa wenye wazo zuri ambalo ni la kibiashara na kusaidia jamii," anasema Dk. Nungu.

Anasema vijana wenye wazo mazuri watapata mafunzo ya miezi sita, ili kuwezesha walichojifunza kuwa uhalisia na kukuza uelewa, kisha kuwekeza kipato chao na taifa, kwenda sambamba na dunia ya kidigitali.

Pia, anautafsiri ni mradi maalumu wa kisayansi, unaobeba wazo la ubunifu kutengeneza ajira na uchumi.

"Tuna shule nane za Dar es Salaam kwenye mradi, pia tano kutoka Arusha. Tunawapa elimu ya ziada kufanya sayansi wanayoisoma kuwa biashara kupitia ubunifu wao," anasema Josephine Sepeku, Meneja wa Mradi huo.

Ofisa Utafiti Mwandamizi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Rodgers Msuya, anasema wizara inatambua mchango wa mradi huo kukuza sayansi na vipaji.

### MALARIA IKOJE?

Mwaka 2017, karibu nusu ya idadi ya watu duniani walikuwa hatarini kuugua malaria.

Pia, katika kundi hilo walioukufa, asilimia 61 au theluthi mbili ni watoto, huku wajawazito na watu walio na mfumo hafifu wa kinga waliangukia katika hatari.

Mwaka 2017 kwa mujibu wa WHO, kuliripotiwa watu milioni 219 waliougua malaria kutoka nchi 87 na inakadiriwa 435,000 walifariki dunia.

Barani Afrika, kunatajwa kuwapo maambukizi asilimia 92 ya malaria duniani. Pia, sehemu kubwa zaidi ya vifo kwa takwimu za mwaka huo, ni zilichangiwa na malaria.

AFYA

# Wakazi Babati katika tabasamu mradi maji tangu kupata uhuru

- Wafurahia kuyaaga maradhi, safari porini
- Kutoka ndoo Sh. 500, leo pipa kujaa Sh.100

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

NI tendo la kihistoria kwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, baada ya wananchi wake tangu Uhuru kupata maji kwa mifumo rasmi.

Hasa mwaka 2019, ndio kumeanzishwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilaya ya Babati, ikianza na vijiji 69 kati ya 102 vilivyokuwapo.

Meneja wa RUWASA, Mhandisi Bakari Mwanyiro, anasema taasisi hiyo ilianza na vijiji 69 na hadi sasa imefikia 75 vimeshapata huduma ya maji, ikiwa sawa na asilimia 73 ya wahitaji wote.

Mhandisi Mwanyiro anasema, upatikanaji maji uko sahihi na kuna zaidi ya wakazi 200,000 kutoka vijiji 75 wanakopata maji, matarajio ni ifikapo mwaka 2025 watafikia asilimia 85 vijiji vyote.

Anaitaja RUWASA kuwa mkombozi wa wananchi, kwa kuwa imeleta matokeo makubwa ndani ya muda mfupi, wastani wa mwaka mmoja.

Ili kulinda vyanzo hivyo vya maji, sheria inataja anayethibika mahakamani kuharibu miundombonu ya maji, yuko hatarini kukabiliwa na faini isiyopungua Sh. milioni tano au kifungo cha miaka mitano jela au vyote kwa pamoja.

### MIFUMO INAYOTUMIKA?

Mtaalamu huyo anasema, wanatekeleza miradi kwa kutumia Mfuko wa RUWASA wakirithi miradi iliyokuwa inasimamiwa na halmashauri za wilaya.

Anaitaja mifumo mingine kwa majina 'P4R' na Programu ya Lipa Malipo kwa Matokeo (PBR), inayolenga kuboresha huduma ya maji, iliyoanzishwa na wafadhili kwa ajili ya ukarabati wa miradi chakavu, iweze kuendelezwa.

Meneja huyo anasema wilaya ya Babati wana miradi mitano inayotekelezwa, na fedha za wahisani, ikilenga kurekebisha miradi chakavu na mtarajio ni kukamilika kabla ya Juni 30 mwaka huu.

Programu ya 'P4R', anaitaja inaangalia kwa jicho endelevu ikifadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), ili kuimarisha miradi iliyoasisiwa na RUWASA, mmoja ni katika kijiji cha Endakiso ni kati ya miradi sita iliyopo.

### MIRADI ILIYOKAMILIKA

Meneja huyo anataja miradi mingine 10 inayoendelea katika mwaka wa fedha uliopo, ikiwamo kijijini Gidas uliokwishakamilika, kati ya mitatu waliyoirithi kutoka Halmashauri ya Wilaya Babati.

Mradi wa maji wa Kijiji cha Endakiso, Mhandisi Mwanyiro anasema wameutekeleza kwa miezi sita kuanzia Juni 2020 hadi Desemba 30 mwaka huo, ujenzi wake ulikadiriwa kugharimu Sh. milioni 234 na walitumia Sh. milioni 172 hadi kukamilika. Hivyo, wameokoa Sh.milioni 62.

Mhandisi Mwanyiro anasema katika mradi huo, wamejenga vituo vinane vya kuchota maji na tanki moja lenye ujazo wa lita 90,000, kwa sasa unatoa maji kwa wakazi zaidi ya 2000.

Gharama zake anasema, walitumia bajeti anayoiita "force account" yaani mafundi jamii na wataalamu wa ndani.

Kijijini cha Gidas, wamerithi mradi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Babati, walioupokea mwaka 2018. Baada ya kukosekana chanzo cha maji, walitafuta mbadala kwa kuchimba kisima cha lita 8000 kwa saa.

Meneja anasema, mradi uliipangiwa bajeti ya Sh. milioni 354, mkandarasi akalipwa Sh. milioni152 na kisima kikachimbwa kwa Sh. milioni 64 mradi ukaanza kutumika tarehe 16, mwezi uliopita, ukiwa umeokoa Sh. milioni 138.

Mhandisi Mwanyiro anasema, tayari wameshajenga vituo 18 vya kuchota maji, wameweka umeme na kujengwa tangi la lita 100,000 na kisima. Tayari mradi unawahudumia wakazi zaidi ya 4,000 wa vijiji vya Gidas na Endiamet.

Anataja mradi mwingine ni waliourithi kutoka Halmashauri ya Wilaya Babati, uliokamilika katika eneo Shaurimoyo na sasa imejengewa tangi la lita 50,000.

> Gharama zake anasema, walitumia bajeti anayoiita "force account" yaani mafundi jamii na wataalamu wa ndani.



Kituo cha Kuchuja Maji Mutuka, wilayani Babati, sehemu ya miradi ilipokuwa inaendelea kuandaliwa mwaka jana, chini ya RUWASA. **PICHA: MAKTABA**

### WANANCHI WANENAVYO

Mkazi wa kijiji cha Gidas, Rebecca Joshua, anaishukuru RUWASA kuwaletea maji safi na salama, kwani awali waliugua tumbo na maradhi kama amiba, kwa kutumia maji ya madimbwi.

Anakiri ni jambo ambalo hawakulitegemea kupata maji hadi mlangoni. Anasema:"Tulikuwa tunatumia maji ambayo watu wanajisaidia na mifugo wanatumia ila sasa hivi tuna raha sana unaweza ukachota hata ndoo mbili ukakaa."

Mkazi mwingine, Gidas Valian mwenye umri miaka 69, anaendeleza ushahidi kwamba walipata shida ya kuamka saa 9.00 usiku kwenda kuchota maji, kwani mchelewaji hakupata maji.

"Usiku tulikuwa tunatembea na tochi. Nilikuwa nikichota maji naficha kwanza, halafu mchana nilikuwa nachota maji ya mifugo," anasema.

Mkazi wa kijijini Endakiso, Halima Dai, bila ya kutaja umri, anajitambulisha alifika kijijini hapo mwaka 1973, hakukuta huduma ya maji, akieleza: "Huko nyuma tulikuwa tunauziwa ndoo moja ya lita 20 Sh. 500, hivi sasa pipa Sh.100 ( ndoo 13)."

Mkazi wa Kijiji cha Maweni, Zuwena Kimaro, anasimulia shida zao hata kuishia kunywa maji ya makorongoni kwa watu maskini, lakini sasa mradi umewakomboa, kwani nyuma aliugua tumbo, Typhod na Amoeba kwa kuwa alikuwa anatumia maji machafu.

### WASIMAMIZI VIJIJINI

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumiaji Maji wa Kijiji cha Endakiso, Said Issa, anasema jukumu lake ni kusimamia mradi uwe endelevu na kupanga bei kwa kuwashirikisha watumiaji.

Issa anasema, mradi unawaonyesha matokeo mazuri pale hata wananchi wanaposhangaa kununua maji ndoo moja ya lita 20 kwa bei Sh. 10.

"Leo tuna uhakika kila mtu kufikishiwa maji nyumbani kwake," anasema Issa, huku akihamasika na wenzake kudhibiti uharibifu wa miundombonu ya maji.

Diwani wa Kata ya Kisangaji, Adam Ipingika, anaahidi kuendelea kutoa elimu ya utunzaji miradi, huku akiazimia kuzisimamia tozo ili kufikia malengo," anasema.

Diwani huyo ana rai kwamba RUWASA isichoke 'wamtue mama ndoo kichwani; walau kila mita umbali 400, ambayo ndio mtazamo wa kisera nchini.

Mwakilishi huyo wa wananchi, anasema walipata athari za kuugua magonjwa kama homa ya matumbo (typhoid) na amiba kutokana na kutumia maji machafu na idadi ya wagonjwa waliongezeka katika zahanati yao, hali iliyobadilika sasa idadi hiyo inashuka.

Anasema, iliendana na taarifa za wanandoa wengi kugombana kwa kisa kuchelewa kuchota maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Shaurimoyo, Dismas Morembwa, anasema kabla ya RUWASA kuwajengea mradi wa maji, wananchi walikuwa wanaenda milimani na walikutana na wanyama wakali.

Morembwa anaaihidi kuitunza miradi, akifafanua wataongeza vituo vya kuchota maji baada ya kukusanya mapato.

AFYA

# Kwanini vidonge vya uzazi vya kinababa ibaki bidhaa adimu ?

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA ya 1800 wakati dunia inakumbwa na mabadiliko ya kijamii na uchumi, ongezeko la watu lilidhaniwa kuwa tishio kwa uhai wa binadamu na mazingira yanayomzunguka.

Wakati huo, mataifa yaliyoendelea yalibuni njia ya kupunguza idadi ya watu, kwa kuhofia siku moja watu wangeshindwa kupata mahitaji yao muhimu kama chakula, elimu na mavazi kutokana na kushindwa kuwamudu.

Hapo ndipo kunaelezwa kwamba, juhudi ziliaanza kufanyika kutafuta njia nzuri bora za kupunguza idadi ya watu kwa kupanga uzazi, kupitia familia.

Hata hivyo, njia zote zilizopatikana zilishindwa kufikia malengo, baada ya kuonekana zipo kwa ajili ya wanawake pekee, huku wanaume zikiwaacha nyuma.

Mwaka 1960 vidonge vya kwanza vya kupanga uzazi vilibadilisha mtazamo wa ulimwengu wakati kilipoletwa katika jamii mnamo miaka ya 1960.

Hivi sasa, vidonge hivyo vinatumiwa na wanawake wapatao milioni 214 duniani kote na kila mwaka, inatumika takriban Dola za Marekani milioni 18,000 (Sh. trilioni 41.4) kuzinunua.

Zaidi ya miongo sita sasa imepita tangu  tangu kuzalishwa vidonge, kuna njia 20 za kupanga uzazi, ambazo Shirika la Afya Duniani (WHO) imeziidhinisha, lakini ni aiba mbili tu zinazoweza kutumiwa na wanaume.

Swali linaloumiza vichwa, ni vipi wataalamu wengi wa afya ni kwa nini katika vidonge hivyo vya uzazi, hakuna vinavyotumiwa na wanaume? C


Profesa Adam Watkins, anasema wazo la kutengeneza vidonge vya mpango wa uzazi kwa wanaume, limekuwapo kwa muda mrefu, kama utengenezaji wa mbinu ya upangaji uzazi kwa wanawake.

Mtaaluma huyo bingwa wa Baiolojia ya Uzazi kutoka Chuo Kikuu cha Nottinghan, Uingereza, anasema  ugumu mkubwa unaoukabili mpango huo ni wakati mwanamke anatoa yai moja kwa mwezi, mwanaume hutoa mamilioni ya mbegu kila siku, hivyo ni vigumu kuzuia.

Anasema, hata kama mwanaume atapoteza asilimia 90 ya uwezo wake wa kuzalisha, bado anaweza kurutubisha yai na hiyo ndio inachangia sababu kidonge chenye ufanisi na salama kwa wanaume hakijatengenezwa.



Jamii ya wanafamilia. **Picha ya chini;** dawa za uzazi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**




**"Nadhani ikiwa haijatengenezwa vyema, imekuwa kwa sababu ya mafanikio ya kidonge cha upangaji uzazi kwa wanawake. Inafanya kazi vizuri na ni bora kwa mtazamo wa kiuchumi.**

"Nadhani ikiwa haijatengenezwa vyema, imekuwa kwa sababu ya mafanikio ya kidonge cha upangaji uzazi kwa wanawake. Inafanya kazi vizuri na ni bora kwa mtazamo wa kiuchumi," anaeleza mtaalamu huyo.

Njia pekee ambazo mwanaume anashiriki katika upangaji uzazi inayotambuliwa na WHO, ni matumizi ya kondomu na kinga  nyinginezo.

"Kwa sababu tofauti, mzigo wa upangaji uzazi ulitwika wanawake," anaongeza na kufafanua, kwamba wanawake pekee ndio wanawajibika katika jukumu hilo, hatua ambayo wengi wanaona sio sawa.

### UHALISIA ULIVYO

Mpango wa uzazi wa zamani katika historia ni kondomu, hii ilianza kutumika miaka mingi na  katika karne ya 18, hatua ya mwisho katika mchakato wa kutafuta mbinu ya kiume ya kupanga ilipatikana. Utaratibu wa upasuaji unaokata uwezo wa uzalishaji.

Halafu, katika nusu ya pili ya karne ya 20, baada ya hatua kubwa kupigwa katika utengenezaji wa kidonge cha wanawake, safari ya kutengeza kinachotumiwa na wanaume ilianza, lakini bado inawaumiza vichwa wanasayansi hao.

Njia ya pili inatajwa ni kuzuia mbegu za kiume zenye afya kuingia ukeni na kuweza kurutubisha yai .Hata hivyo, tafiti zinazolenga kubuni kidonge cha kiume zimeathiriwa na changamoto nyingi, ikiwamo zinazosababishwa na viungo vyake.

### WANAUME WAJARIBIWA

Mwaka 2016, kuna utafiti uliofanyika kuliwadunga wanaume sindano za 'testosterone' na 'projestojeni'sawa na homoni zilizopatikana kwenye kidonge cha kike, lakini ilipigwa marufuku mapema .

Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya kubainika kukuwapo na athari kama vile chunusi kwenye ngozi, shida za mhemko na wanaume waliona ni kali sana na haiwezi kuvumilika, kwa hivyo uchunguzi ulifutwa.

"Wataalamu wengi wanaweza kuona athari hizi kama ndogo ikilinganishwa na zile zinazopatikana kwa wanawake wanaotumia kidonge, pamoja na wasiwasi, kuongezeka kwa uzito, kichefuchefu, maumivu ya kichwa, kupunguza libido na kuganda kwa damu," anasema Profesa Watkins.

Kondomu inatajwa hutumiwa sana na wanaume, lakini haina ufanisi kama vidonge na Dk. Lisa Campo-Engelstein, Mkurugenzi wa Taasisi ya Maadili na Afya ya Binadamu katika Chuo Kikuu cha Texas, Marekani, anasema kukosa kidonge cha kupanga uzazi kwa wanaume, sio kushindwa sayansi ya kupata kidonge hicho.

"Ni wazi kwamba kutokuwepo kwa kidonge cha wanaume cha kupanga uzazi sio kwa sababu ya suala la kisayansi, lakini kwa ajili ya suala la kijinsia, la kanuni za kijamii. Kazi hii ilikuwa ya wanawake tu," Campo-Engelstein anasema.

Anaongeza:"Siku hizi wanawake hubeba mzigo mkubwa wa kifedha na kiafya unaohusiana na upangaji uzazi. Kwa ujumla, njia za kike huwa za bei ghali zaidi kuliko za kiume kwa sababu nyingi zinahitaji kumuona daktari zaidi ya mmoja na nyingine zinahusisha dawa zinazofaa kumezwa kwa kipindi fulani,"

Dk. Engelstein anatoa wito wa kuwapo kwa kidonge cha kupanga uzazi kwa wanaume hivi karibuni ili kuwaepusha wanawake kubeba jukumu hilo zito.

***Kwa mujibu wa BBC.***



# Tanzania kukabidhiwa uenyekiti nchi zinazozalisha madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA inatarajiwa kukabidhiwa leo uenyekiti wa Jumuiya ya nchi wanachama wanaozalisha madini ya almasi Afrika (ADPA), kwa mwaka mmoja kutoka Namibia, huku ikijivunia kutumia nafasi hiyo kuhamasisha masoko ya kuuza madini ndani ya bara hilo.

Akifungua mkutano wa saba wa mawaziri jana, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema makabidhiano hayo yatafanyika kwa njia ya video na balozi wa Tanzania nchini Namibia, ambaye atakayepokea kwa niaba ya Waziri wa Madini wa Tanzania.

Alisema kuwa mkutano huo utahusisha ushiriki wa mawaziri na wataalam wa madini katika nchi 12 wanachama na utajadili masuala mbalimbali katika sekta ya madini.

Alitaja nchi hizo kuwa ni Angola, Kongo, Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe, Tanzania, Cameroon, Afrika ya Kati, Ghana, Togo, Guinea na Sierra Leone. "Kutakuwa na waangalizi kutoka nchi saba ambazo ni Algeria, Jamhuri ya Kongo, Code D' Ivore, Gabon, Liberia, Mali na Mauritania, kesho (leo) ni mkutano wa mawaziri wa kutoa uamuzi kwenye masuala yatakayokuwa yamejadiliwa na wataalam," alisema.

Alisema majadiliano hayo yatatoa fursa ya kubadilishana uzoefu kwa nchi wanachama kuhusu usimamizi wa sekta ya madini na kuimarisha utendaji katika wizara ambayo wanasimamia. "Katika uenyekiti wetu tutajadili na kuhakikisha kwamba tunaboresha mifumo ya Jumuiya ya ADPA ili kuwa na manufaa kama ambavyo inakusudiwa, na katika kipindi chetu cha uenyejiti, tunaenda na dhana ya kuwa na masoko ndani ya Afrika ya kuuza madini na Tanzania imekuwa mfano mzuri wa kuanzisha masoko kila kona ya nchi," alisema.

Pia, mkutano uliofanyika Namibia ulilenga Afrika yenyewe ianzishe masoko yake hasa ya madini ya almasi ambapo kwasasa almasi yote inayovunwa duniani inauzwa Ubelgiji.

"Tunafikiri nchi za Afrika kuwa na masoko yetu pamoja na almasi tunazochimba yafanyiwe biashara hapa ndani Afrika na kuongezewa thamani, ili tuhame kutoka kwenye nchi zinazozalisha malighafi kutoka nchi za wenzetu na sisi tupeleke bidhaa ambazo zimetengenezwa kwenye masoko ya kimataifa," alisema.

Alisema ni wakati wa nchi za Afrika kuwa na sauti moja kwenye rasilimali zao na kuwa na mfumo wa kisheria unaofanana.

"Kama kuna mwekezaji atakuja Tanzania akute setup akienda nchi nyingine kama Mali, Afrika Kusini akute setup ya aina hiyo, hatuwezi kufanya peke yetu kama nchi, ni sehemu ya Afrika tushirikiane na wenzetu," alisema.

Alifafanua kuwa Tanzania ina mgodi mkubwa wa dhahabu wa William Daimond ambao upo Kishapu mkoani Shinyanga na uzalishaji wake umefika kwa kiwango cha juu cha kalati 497,000 kwa mwaka na uzalishaji wa namna hiyo mara ya mwisho umetokea mwaka 1977.

"Mgodi huo umewahi kuzalisha kalati 370,000 kwa kipindi hicho, hapa katikati uzalishaji ulishuka kutokana na marekebisho ya sheria sasa uzalishaji umepanda hadi kufikia 497,000," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na ugonjwa wa Corona bei ya almasi duniani ilipungua na uzalishaji ulishuka kwenye mgodi huo na wanaangalia hali itakavyokuwa ili mgodi huo urudi kwenye uzalishaji.

"Tunaangalia mapato tunayopata kwenye sekta ya madini yanayoongoza ni dhahabu na yanayofuata ni almasi, ndio vinafuata vitu vingine na madini ya ujenzi, masoko yapo kila mahali," alisema.



Mdau wa elimu ambaye pia ni mwanachuo wa mwaka wa tatu Chuo cha Uhasibu Arusha, Emmanuel Bundala (aliyevaa kofia), akishiriki kula chakula cha pamoja na baadhi ya vijana wanaoishi kwenye mazingira hatarishi wa jijini Dodoma jana, baada ya kuwapatia misaada mbalimbali ikiwamo elimu ya ushauri nasaha kwa ajili ya maisha yao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Baraza la vyama vya siasa laomba kukutana na Rais

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Vyama vya Siasa limemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kukutana na viongozi wa baraza hilo ili kuzungumza nao na kuwapa nasaha zake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa baraza hilo, John Shibuda, alisema tasnia ya siasa na wadau wake ipo tayari kushirikiana na serikali katika kudumisha amani, upendo na mshikamano wa kushauriana na kukosoana.

"Tukosoane sisi kwa sisi, hii iwe ni badala ya baadhi ya wadau wa siasa kutumia marafiki wa Tanzania nje wawe ndio sikio sikivu kwa maumivu ya wavaa viatu vya siasa za Tanzania," alisema.

Alisema umuhimu wa kipekee wa fumbuzi za kuondoa kusigana kati ya wadau wa vyama hivyo na mamlaka za dola sasa ni wakati wa kuwapo kwa vikao vya baraza hilo.

"Hivi vifanyike kwa mujibu wa sheria na kanuni za vyama vya siasa Tanzania, na hii iwe nia ya serikali ya awamu ya sita katika ufufuaji uhai wa demokrasia ya vyama vingi hapa nchini," alisema.

Aliwataka viongozi na watumishi wa serikali kupandisha viwango vya sifa ya kukweza kwa kuwa Tanzania kuna mfumo wa vyama vingi na vipatikane na haki zote za Katiba ya nchi.

Alimpongeza Rais Samia kwa kuwa ngao kinga dhidi ya umma kwa kuleta matokeo chanya kupitia hotuba zake.

"Matendo haya ni uamsho mpya unaokweza morali na kukuza ari mpya ya umma kuwa rafiki na serikali hii ya Rais Samia, nampa hongera sana kwa hatua zake alizoelekeza zitimizwe na utumishi wa awamu ya serikali yake," alisema.

Akizungumzia mambo ya kumuenzi Hayati Rais John Magufuli, Shibuda alisema ataenziwa kwa mambo mengi aliyoyafanya kwa nchi yake na Watanzania kwasasa wanafahamu ukombozi wake hautowajibikiwa kifikra na matendo na taasisi za nje.

Alisisitiza kuendelezwa kwa vitendo imani ya uhuru ni kazi.

"Maumivu ya leo ni furaha ya kesho, kwa hiyo tunuku zake tuzizawadie kwa kukubali Rais Samia inapompasa atunyweshe dawa chungu tuwe tayari kuinywa na tupongeze anatupatia tiba salama kwa maendeleo ya nchi yetu," alisema.

# Watanzania watakiwa kuwa na imani na Samia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya wazazi Taifa ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Edmund Mndolwa, amesema kuwa wanaimani kubwa na uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, na kuwataka wanaCCM, pamoja na Watanzania kumuunga mkono ili akamilishe mambo yaliyoanzishwa na mtangulizi wake.

Dk. Mndolwa aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema wanachama wa chama hicho wana wajibu wa kumuunga mkono katika mkutano mkuu wa dharura wa CCM, na kumpitisha kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa.

"Hayati Magufuli nchini Tanzania alikuwa kama Musa wetu kwenye Biblia na mama Samia Suluhu Hassan ni Joshua wetu wameanza kasi ya maendeleo ya nchi pamoja na sasa Mungu kamchukua Musa wetu na kumuacha Joshua," alisema Dk. Mndolwa.

Alisema pia Rais Samia ni mtu sahihi kushika nafasi iliyoachwa na Hayati Magufuli kutokana na kushiriki katika kuandaa Ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

Alisema, wakati wa kuandaa Ilani ya uchaguzi ya CCM, Rais Samia alikuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM, Philipo Mangula.

"Wakati wa kuandaa ilani yetu mama Samia alikuwa makamu mwenyekiti wa mzee Mangula na katika kundaa wakati fulani yeye ndiye alikuwa anachukua jukumu hilo kutokana na afya ya mzee Mangula hivyo kutokana na hali hiyo yeye anayafahamu mambo mengi katika Ilani yetu," alisema Dk. Mndolwa.

Alisema kuwa, kutokana na hali hiyo wana CCM pamoja na Watanzania wanatakiwa kumpa ushirikiano mkubwa ili kukamilisha mambo mbalimbali yalipo kwenye Ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

"Pia tunatakiwa kumuenzi hayati Rais Magufuli kwa kufanya kazi kama ilivyokuwa kaulimbiu yake ya hapa kazi tu ili mama Samia kazi yake ya kulinda uchumi wa kati tulioufikia upande zaidi ya hapa," alisema.

Kadhalika, alimpongeza Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kwa kuteuliwa na kuapishwa kushika nafasi hiyo na kwamba Jumuiya hiyo pamoja na wanachama wake watampa ushirikiano katika utendaji wake.

Hata hivyo, alisema wito wake kwa Watanzania pamoja na viongozi mbalimbali ni kuendelea kulinda Muungano, kufanya kazi kwa bidii na kumuunga mkono Rais Samia.








Meneja wa Kampuni ya Kapunga Rice Ltd, Sunil Tayal (kushoto), akikabidhi kuku kwa mmoja wa watoto yatima wa kituo cha kulelea yatima cha Iwambi, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wataka picha ya JPM kwenye noti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeombwa kuchapisha noti mpya zenye picha ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, kwa ajili ya kumbukumbu na kuenzi kazi nzuri alizolifanyia taifa wakati wa uhai na uongozi wake.

Pia imeombwa kuchapisha noti zingine zenye picha ya Rais wa sasa, Samia Suluhu Hassan, ili iwe kumbukumbu yake ya kuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Tanzania.

Ombi hilo lilitolewa juzi jijini Mbeya na Kamati Tendaji ya Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za kifedha na Huduma na Ushauri (TUICO) wakati wa kuhitimisha siku 21 za maombolezo ya kitaifa ya kifo cha Hayati Dk. Magufuli.

Akizungumza wakati kutia saini kitabu cha maombolezo juzi, Katibu wa TUICO Mkoa wa Mbeya, Melboss Kapinga, alisema kamati hiyo inapendekeza picha ya Hayati Magufuli ichapishwe kwenye noti ya Sh. 5,000.

"Lakini pia tunapendekeza ikiwezekana ichapishwe noti ya Sh. 20,000 au 6,000 na kuwekwa picha ya Rais Samia ili iwe kumbukumbu kwake kutokana na kuwa Rais wa kwanza mwanamke katika nchi yetu," alisema Kapinga.

Mwenyekiti wa TUICO Mkoa wa Mbeya, Luka Mwasimba, alisema Dk. Magufuli katika uhai wake, alifanya mambo makubwa ya maendeleo ambayo yanatakiwa kuwekewa kumbukumbu ili hata vizazi vijavyo vimkumbuke.

Alisema kamati hiyo inapendekeza picha yake iwekwe kwenye noti ya Sh. 5,000 kwa sababu ni miongoni mwa noti kubwa katika fedha za Kitanzania huku akidai kuwa picha ya Rais Samia inapendekezwa iwekwe kwenye noti mpya kabisa ambayo haijawahi kuchapishwa.

"Katika historia ya taifa letu hatujawahi kuwa na Rais mwanamke, hivyo tunapendekeza picha yake iwekwe kwenye noti mpya kabisa ambazo tunapendekeza iwe 20,000 au 6,000," alisema Mwasimba.

Nao baadhi ya wajumbe wa Kamati Tendaji ya TUICO Mkoa wa Mbeya walieleza namna ambavyo watamkumbuka hayati Dk. Magufuli huku wakimwombea heri Rais Samia ili aliongoze vyema taifa.

Mmoja wa wajumbe hao, Alex Kilamlya, alisema Hayati Dk. Magufuli alifanya mambo mengi wakati wa uhai wake, hivyo anatakiwa kuenziwa kwa namna yoyote ile ikiwamo Watanzania kufanya kazi kwa bidii.

Alisema kiongozi huyo ameliacha taifa likiwa limefikia hatua ambayo ni nzuri na kila mmoja anatakiwa kuhakikisha analifanyia taifa mambo mazuri ikiwamo kulipa kodi kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kimkakati iliyoanzishwa pamoja na uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Naye Anna Mwakyembe alisema ana uhakika Rais Samia ataliendeleza taifa kutokana na kwamba alikuwa anafanya kazi na Hayati Dk. Magufuli na kutokana na hali hiyo, ana uwezo na uzoefu wa kutosha wa kushika nafasi hiyo.

Aliwataka Watanzania kuendelea kumpa ushirikiano Rais Samia na serikali yake ili aendeleze miradi ambayo waliianzisha pamoja na hayati Dk. Magufuli.

# Watoto yatima wakatiwa bima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATOTO yatima 25 wanaolelewa katika Kituo cha Watoto Iwambi, jijini Mbeya, wamekatiwa bima za afya na kampuni ya Kapunga Rice Limited ili kuwahakikisha huduma za matibabu.

Akizungumza juzi wakati wa kukabidhi msaada huo wa bima ya afya ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) katika kituo hicho kinachomilikiwa na Kanisa la Moravian, Meneja wa Kapunga Rice, Sunil Tayal, alisema Sh. milioni tatu zilitumika kukata bima na kununua mahitaji mengine ambayo wameyatoa.

Meneja Tayal alisema mahitaji mengine waliyoyatoa ni pamoja na mchele, maharage na sabuni ambavyo walivikabidhiwa kwa msimamizi wa kituo hicho.

"Kampuni ya Kapunga Rice Limited imekuwa na utaratibu wa kushiriki na kusaidia shughuli za kijamii ikiwemo ukarabati wa miundombinu ya elimu wilayani Mbarali na ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kapunga, tumeona kutanua wigo wa kuhudumia jamii ambapo sasa tumetoa msaada wa kuwakatia bima za afya watoto wote na kuwapatia mahitaji mengine muhimu, kiu yetu ni kuifikia jamii yote ya Mbeya alisema," alisema Tayal.

Aliongeza kuwa mwaka ujao wataendelea na utaratibu wa kuwakatia bima watoto yatima katika vituo vingine na hao walionufaika mwaka huu wataendelea kupata huduma hiyo lengo likiwa ni kuwahakikisha wanapata huduma bora za matibabu kwa wakati na uhakika.

Msimamizi wa Kituo hicho, Sabina Siwale, alisema awali watoto hao walikuwa wanatibiwa na fedha na kwamba walikuwa wanatumia gharama kubwa.

Alitolea mfano wa miongoni mwa watoto katika kituo hicho aliugua na alipopelekwa hospitali alitumia zaidi ya Sh. 800,000 kutibiwa.

Alisema kutolewa kwa bima za afya kutapunguza gharama za matibabu ambapo hapo kabla walitumia pesa taslimu ili kupata matibabu pindi wanapougua.

# RUWASA yasikia kilio cha wananchi wa vijijini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya Nipashe kuripoti taarifa ya wananchi wa vijiji vinne vya Kata ya Tembela katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, maofisa wa Wakala wa Majisafu na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wameanza harakati za kuwapelekea maji wananchi hao.

Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mbeya, Mhandisi Vivian Mndolwa, alisema awali vijiji hivyo vilikuwa vinatumia maji yaliyokuwa yanasukumwa na pampu lakini pampu hizo ziliharibika na kusababisha wananchi hao kukosa maji.

Alisema walijaribu kuzitafuta pampu za aina hiyo lakini hazikupatikana kutokana na kutokuwapo tena kwenye soko, hivyo wakaanza kutafuta chanzo kipya cha maji ili kuwahudumia wananchi hao.

Mndolwa alisema walijaribu kutumia chanzo wananchotumia wananchi wa Kata ya Igoma lakini wakabaini kuwa hakitoshelezi hasa kipindi cha kiangazi kwa kuwa maji hupungua na wakaachana nacho na kuendelea kutafuta kingine.

"Tumejaribu chanzo ambacho kipo jirani na kata hiyo lakini tumebaini kuwa maji hayo hayawezi kupanda, sasa hivi usanifu ambao unafanywa na ofisi ya meneja ni kutumia pampu maana vyanzo vingi viko mabondeni, tutasukuma maji mpaka kwenye matangi kisha kuyasambaza kwa wananchi," alisema Mndolwa.

Alisema usanifu wa mradi huo utakamilika mwaka huu ili utekelezaji uanze mwakani na kwamba mradi huo umeshaingizwa kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

Diwani wa Tembela, Juma Mwakalobo, maarufu kwa jina la 'Mwadangala' alisema kata yake ina vijiji sita ambavyo ni Shibolya, Gari-Jembe, Simambwe, Ilembo-Usafwa, Isoha-Njiapanda na Ngoha.

Alisema kati ya vijiji hivyo ni viwili pekee ambavyo angalau vinapata maji ambavyo ni Gari-Jembe kinachopata maji kutoka kwenye mradi unaohudumia Shule ya Wasichana ya Gari- Jembe na kijiji cha Ngoha ambacho kinapata huduma hiyo kutoka katika Kata ya Igoma.

Baadhi ya wanawake wa vijiji hivyo walisema tatizo hilo la maji limekuwa likisababisha kuhatarisha maisha yao kutokana na kuamka usiku na kutembea kwenye maeneo yaliyojaa misitu.

Mmoja wa wanawake hao, Gulila Kasege, mkazi wa Kijiji cha Simambwe alisema kutoka nyumbani kwake mpaka maji yanakopatikana ni zaidi ya kilomita tatu na kuna milima na vichaka ambavyo vinatishia usalama wake.

Alisema wakati mwingine huwa wanaviziwa na vibaka hasa kipindi ambacho mahindi yamekuwa marefu hali ambayo inawafanya wawe wanahamasishana kwenda kwa makundi ili kuepuka kudhurika.

"Huwezi kwenda peke yako kwa hiyo huwa tunaitana angalau tuwe watano ndiyo tushuke kule bondeni kuchota maji. Lakini pia sasa hivi ni msimu wa mvua kuna utelezi njiani unaweza ukateleza ukaumia na ukiwa mjamzito mimba inaweza ikatoka huko huko," alisema Gulila.

## Wazazi wakumbushwa umuhimu wa elimu kwa watoto

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Kamati ya Maendeleo ya Elimu Wilaya ya Kusini Unguja, wametakiwa kusimamia majukumu yao pamoja na kuwaelimisha wazazi umuhimu wa elimu kwa watoto wao.

Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, aliyasema Kitogani wakati akizungumza na viongozi, wazazi, walezi na wadau wa elimu baada ya kuzindua kamati ya elimu ya wilaya yenye lengo la kusimamia masuala ya elimu wilayani humo.

Alisema ndani ya miaka minne mfululizo mkoani humo sekta ya elimu imekumbwa na changamoto ya kupata matokeo mabaya ya mitihani ya kidato cha nne na kuundwa kwa kamati hiyo kutasaidia kuinua kiwango cha ufaulu mwaka huu.

Aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kuwa wazalendo kwa kusimamia maazimio yote yatayopitishwa katika kikao hicho ili yawe mwongozo na kuachana na muhali katika kusimamia majukumu yao na kufikia lengo la kamati hiyo.

Alisema kuwa serikali inategemea kupata vijana wengi wenye sifa na uwezo wa kulitumikia taifa hivyo ina jukumu la wazazi kutoa ushirikiano ili lengo la watoto hao liweze kufikiwa hali itakayowawezesha kufanya vyema katika mitihani yao.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Rashid Makame Shamsi, alisema sekta ya elimu katika wilaya hiyo inaweza kuimarika zaidi iwapo walimu, wazazi na walezi watatoa ushirikiano kwa wajumbe wa kamati hiyo ili kutekeleza vyema majukumu yao na hatimaye kuleta mabadiliko ya kielimu ndani ya wilaya hiyo.

Alisema lengo la kuanzishwa kamati hiyo yenye wajumbe 31 ni kusimamia masuala yote ya elimu kwa dhamira ya kuondoa matokeo mabaya na kwamba ni vyema kwa wazazi kuipa ushirikiano kamati hiyo ili kuwajibika ipasavyo.

# Rais Mwinyi ataja sababu mafuta ya kula kupanda

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kupanda kwa bei ya mafuta ya kula kunatokana na baadhi ya nchi duniani kukabiliwa na janga la ugonjwa wa corona.

Aliyasema hayo juzi Ikulu mjini Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari alipoulizwa swali sababu ya kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali hasa mafuta ya kula.

Alisema sababu za msingi za bidhaa kupanda bei ni kutokana na nchi hizo kukabiliwa na corona na uzalishaji hauko vizuri katika nchi hizo na ndio maana usafirishaji umekua mdogo kuliko mahitaji na wafanyabiashara wanapandisha bei huko zinakotoka.

Alisema licha ya sababu hizo za msingi zilizosababisha kupanda kwa bei ya baadhi ya bidhaa, lakini kuna tabia ya wafanyabiashara kutaka kupata faida za ziada kwa kupandisha bei hasa kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na waandishi wa habari, Ikulu Zanzibar juzi. PICHA: IKULU

Dk. Mwinyi alisema tayari dalili zimeshaanza kuonekana za wafanyabiashara kuanza kupandisha bei za bidhaa wakitarajia kwamba Ramadhani inakuja ili wapate faida zaidi jambo ambalo si zuri kufanyika mwezi huo mtukufu.

Aliwasihi wafanyabiashara kutambua kwamba wakati wa Ramadhani ni wa kuvuna thawabu kwa kuwatumikia watu kwa kupunguza faida wanazoziweka ili watu waweze kufunga vizuri na kumcha Mola wao badala ya kuanza kupandisha bei za bidhaa kama walivyoanza kufanya hivi sasa.

Alisema anatambua hivi sasa dunia imeingia katika changamoto ya kibiashara kutokana na maradhi ya Covid-19 na kusababisha bidhaa nyingi kuwa adimu huko zinakotoka na usafirishaji kuongezeka gharama jambo ambalo haliepukiki.

Ikiwa bado wiki moja kuanza kwa mfungo Ramadhani bei za bidhaa za vyakula zimeanza kupanda kiroba cha unga wa ngano cha kilo 25 kinauzwa Sh. 33,000 badala ya 28,000,

Mafuta ya kula dumu la lita 20 ni Sh. 57,000 badala ya 44,000 na sukari kiroba cha kilo 50 kinauzwa Sh. 84,000 badala ya Sh. 79,000.

# JUWAVIZA yalalamika wafanyakazi baa kukamatwa

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Magharibi (B) Unguja imefanya makosa kuwakamata wafanyakazi wa baa na kuchukua vinywaji wakiwa na askari wenye silaha za moto kabla ya kesi ya kupinga ongezeko la tozo la leseni kutolewa hukumu na Mahakama Kuu.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wauza Vinywaji Zanzibar (JUWAVIZA), Hussen Ali Kimti, alipokuwa akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari kuhusu operesheni ya ukaguzi wa leseni za baa iliyofanyika juzi Zanzibar.

Alisema kwa mujibu wa taarifa walizopokea kutoka kwa wanachama, askari wa polisi na vikosi vya SMZ wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Magharibi (B) Unguja, Hamida Mussa Khamis na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa la Halmashauri ya wilaya hiyo walipita katika baa mbali mbali na kuwakamata wafanyakazi na kuchukua vinywaji.

"Jambo la kusikitisha katika operesheni hiyo askari walikuwa na silaha za moto wengine wakiwa wamefunika nyuso kwa kutumia ninja baadhi ya milango ya baa ilivunjwa na kuondoka na vinywaji," alisema Kimti.

Alisema katika misingi ya utawala bora viongozi hawakupaswa kwenda kufanya operesheni kama hiyo wakati kesi ya kupinga ongezeko la tozo ya leseni za baa ikiendelea kusikilizwa Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Kimti alisema JUWAVIZA iliamua kufungua kesi baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara maalum kutunga kanuni kupitia Sheria ya vileo namba 9 ya mwaka 2020 na kupandisha tozo ya leseni kutoka Sh. 2,000,000 mpaka Sh. milioni 4.8 kwa mwaka.Alisema wakati wamiliki wa baa wakitakiwa kulipa kiwango hicho waingizaji wa vileo wametakiwa kulipa Sh. milioni 35 badala ya Sh. milioni mbili pamoja na baa kutakiwa ziwe umbali wa mita 1,000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama nyumba za ibada, shule, madrasa na hospitali.

"Tumesikitishwa sana na viongozi wetu kutumia nguvu kubwa wakati sisi tunafanya biashara halali lazima wafahamu serikali yoyote duniani inaendeshwa kwa kutumia kodi sisi hatupingi kulipa kodi tunapinga ongezeko la kodi kwa zaidi ya asilimia 180 bila ya kushirikishwa."

Kimti alisema sheria za kodi lazima ziwe rafiki kwa walipa kodi kama wanavyosisitiza viongozi wa kitaifa akiwamo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussen Ali Mwinyi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan."Kuna watu wanaonekana wanania mbaya na nchi yetu, wamekusudia kuleta mkanganyiko katika jamii serikali lazima ichukue hatua dhidi ya viongozi kama hao," alisema Kimti ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya.Alisema wakati akizindua Baraza la Wawakilishi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussen Ali Mwinyi, alisema sheria kadamizi za kodi lazima zifanyiwe marekebisho ili ziwe rafiki kwa walipa kodi Zanzibar.

Upande wake mmiliki wa baa, Catelina Peter Nao, alisema haikuwa mwafaka wafanyakazi wa baa kukamatwa na wengine vinywaji kuchukuliwa na kuwekwa chini ya ulinzi na askari wenye silaha za moto.

Alisema serikali inapaswa kuchunguza tukio hilo kwa sababu limeleta hofu kwa wamiliki wa baa pamoja na kwenda kinyume na maagizo ya viongozi wa kitaifa ya kuwataka watendaji wakuu kuweka mazingira mazuri kwa walipa kodi.Hata hivyo, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi (B), Unguja Abdalla Said Natepe, alipoulizwa madhumuni ya operesheni huyo alisema msemaji ni Mkuu wa wilaya na Mwenyekiti wa Kamati ya ulinzi na usalama Hamida Mussa Khamis

Upande wake Mkuu wa Wilaya Hamida alisema operesheini hiyo imefanyika baada ya kupokea orodha ya baa zilizokata leseni kutoka bodi ya vileo Zanzibar kabla ya mwaka wa fedha kumalizika pamoja kujitokeza vitendo vinavokwenda kinyume na maadili na kufanyika baa na baadhi ya nyumba za kulala wageni.

Alisema kuna baadhi ya baa zimebainika kufanya biashara bila ya kuwa na leseni, nyumba za kulala wageni kutumika kwa biashara ya ngono, kumbi ya disco, casino kuanzishwa katika makazi ya watu bila ya leseni katika mtaa wa Mbweni Matrekta na makahaba kutumia baa kama kichaka cha kujificha.Hata hivyo, alisema kama kuna watu wanapinga tozo kubwa za leseni za baa wanapaswa kukaa pamoja na Bodi ya udhibiti wa vileo Zanzibar kuzungumza, lakini viongozi wa wilaya na halmashauri kazi yao kusimamia sheria.Hamida alikanusha askari kutekeleza operesheni hiyo wakiwa wameficha sura kwa kutumia ninja, kuvunja milango kama ilivyodaiwa na jumuiya ya wauza vinywaji Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

Nafasi za Kazi ualimu diploma science/math/IT 0715382833

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA INA VYUMBA VIWILI IPO KIJITONYAMA PLOT NAMBA 712/1 BLOCK 46 DAR ES SALAAM BEI 300M,MAZUNGUMZO YAPO.

## KIWANJA KINAUZWA - 1000SQM

Kipo Mbezi Luis 4 km toka Stand ya Mabasi ya Magufuli kina majengo 2, na kina hati (Offer ya miaka 99). Mawasiliano: 0712 600007 / 0777 655007. Bei maelewano.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 2 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**ANDREW MICHAEL NGIRWAMUNGU**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**EDITH NGIRWAMUNGU & ANITA LUKYAA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 29th Mwezi wa APRIL, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 30th Mwezi wa MARCH, 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI KIAPO

Mimi FATUMA MOHAMEDI NDARO wa SIMU NA. 0715-804071 TANGA, Muislam mtu mzima, mwenye akili zangu timamu bila kushawishiwa na mtu yeyote kwa hiari yangu mwenyewe ninaapa na kuthibitisha haya yafuatao:-

1. KWAMBA Mimi FATUMA MOHAMEDI NDARO ni mmiliki wa kiwanja Plot No.105 BLOCK "D" eneo la KANGE TANGA.
2. KWAMBA Kwa bahati mbaya Hati ya umiliki wa kiwanja hicho umepotea nimefanya juhudi ya kuutafuta mkataba huo imeshindikana kuupata.
3. KWAMBA Nimefika kituo cha Polisi na kupewa Loss report namba TAN/IR/156/2020.
4. KWAMBA Ninauomba Uongozi wa Ardhi utambue kuwa Hati ya Umiliki wa kiwanja hicho imepotea ninaomba unisaidie kupata hati nyingine kwa jina la FATUMA MOHAMEDI NDARO.

**UTHIBITISHO.**
Nathibitisha kuwa yote niliyotamka ni ya kweli kweli tupu kwa kadri nijuavyo sharia za Viapo.
**MBELE YA: R.M KOMBO**
**CHEO: HAKIMU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI KIAPO

Mimi FATUMA MOHAMEDI NDARO wa SIMU NA. 0715-804071 TANGA, Muislam mtu mzima, mwenye akili zangu timamu bila kushawishiwa na mtu yeyote kwa hiari yangu mwenyewe ninaapa na kuthibitisha haya yafuatao:-

1. KWAMBA Mimi FATUMA MOHAMEDI NDARO ni mmiliki wa kiwanja Plot No.55 BLOCK "A" eneo la MARTIN'S SHAMBA TANGA.
2. KWAMBA Kwa bahati mbaya Hati ya umiliki wa kiwanja hicho umepotea nimefanya juhudi ya kuutafuta mkataba huo imeshindikana kuupata.
3. KWAMBA Nimefika kituo cha Polisi na kupewa Loss report namba TAN/IR/156/2020.
4. KWAMBA Ninauomba Uongozi wa Ardhi utambue kuwa Hati ya Umiliki wa kiwanja hicho imepotea ninaomba unisaidie kupata hati nyingine kwa jina la FATUMA MOHAMEDI NDARO.

**UTHIBITISHO.**
Nathibitisha kuwa yote niliyotamka ni ya kweli kweli tupu kwa kadri nijuavyo sharia za Viapo.
**MBELE YA: R.M KOMBO**
**CHEO: HAKIMU**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS TO APPEAR**
**(RULE 1, ORDER V.CPC & ACT NO.49 OF 1966)**
**IN THE DISTRICT COURT (RESIDENT MAGISTRATE) OF ……TANGA……….**
**DISTRICT….TANGA……**
**CIVIL CASE NO…….12……OF 2020…….**
**GOSBERT NICHOLAUS MWAISAKA ….PLAINTIFF**
**VERSUS**
**IBONIKE ENTERPRISES……….DEFENDANT**
**TO IBONIKE ENTERPRISES AMIL VAI GROUP**
**P.O BOX- DAR ES SALAAM**

Whereas the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim, the particulars of which are set out in the copy of plaint with annexure hereto attached.

**YOU ARE HEREBY SUMMONED** to appear in this Court in person or by an Advocate duly instructed and able to answer all material questions relating to the suit or who shall accompanied by some person able to answer all such question, on the ..8...day of…April..2021..

At 8.00 O'clock forenoon, to answer the claim, and as the day fixed for your appearance as appointed for the final disposal of the suit, you must be prepared to produce on that day all the witnesses upon whose evidence and all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.

**TAKE NOTICE,** that if you do not appear on the day before mentioned, the court shall upon proof of service of the summons, by affidavit or oral evidence pronounce judgments against you.

**GIVEN** under my hand and the seal of the Court this..30..day of March 2020

**DISTRICT/RESIDENT MAGISTRATE**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Marais SADC kujadili mzozo Msumbiji

**Maputo,** MSUMBIJI

JUMUIYA ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), imesema marais wa nchi sita za kanda hiyo, watafanya mazungumzo ya dharura kuhusu mzozo unaoendelea nchini Msumbiji.

Mazungumzo hayo yatafanyika katika mji mkuu wa Msumbiji, Maputo, leo.

Marais wa Msumbiji, Malawi, Tanzania, Botswana, Afrika Kusini na Zimbabwe.

Jumuiya ya SADC yenye nchi 16 wanachama, ilisema mkutano huo utahusu hatua za kuukabili ugaidi nchini Msumbiji.



Wanamgambo wenye mafungamano na kundi linalojiita Dola la Kiislamu, walifanya uvamizi na kuuteka mji wa Palma, mnamo Machi 24, mwaka huu.

Watu kadhaa waliuliwa na maelfu kulazimika kukimbia mji huo.

Mwenyekiti wa SADC, Rais wa Botswana, Mokgweetsi Masisi, alisema mashambulizi hayo yanatishia amani na usalama wa Msumbiji, eneo zima na jumuiya ya kimataifa. **DW**



Picha iliyopigwa kwa juu ikionyesha athari za mafuriko na kusababisha barabara kuharibika, nyumba kufunikwa na tope kutokana na mvua kubwa, zilizoikumba kisiwa cha Flores, Jimbo la Nusa Tenggara, nchini Indonesia, juzi. **PICHA: REUTERS**

## Misri, Ethiopia, Sudan zashindwa kukubaliana

**Kinshasa,** DRC

MAZUNGUMZO ya hivi punde kati ya Misri, Ethiopia na Sudan kuhusu matumizi ya maji ya Mto Nile, kutumiwa kwenye bwawa kubwa la kuzalisha umeme nchini Ethiopia, yamemalizika bila ya makubaliano yoyote.

Wawakilishi wa nchi hizo tatu, walikutana kwa mazungumzo ya kutafuta mwafaka kuhusu mvutano huo jijini Kinshasa nchini DRC, yalimalizika juzi, bila ya maelewano.

Wizara ya Mambo ya nje ya Misri ilisema, mazungumzo hayo yalivunjika baada ya Ethiopia kukataa pendekezo la Sudan, kutaka wasuluhishi wa kimataifa kuhusishwa katika mazungumzo hayo. Ilibainika kuwa Ethiopia haitaki Marekani, Umoja wa Ulaya (EU), Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU), kuhusishwa katika mazungumzo hayo, msimamo ambao Sudan na Misri zilisema, Ethiopia haionyeshi utashi wa kisiasa kuhusu mvutano huo.

Ethiopia kwa upande wake haijasema chochote kuhusu kuvunjika kwa mazungumzo hayo, ingawa imekuwa ikisisitiza kuwa mradi wake unalenga kuimarisha uchumi na kuzalisha umeme kwa ajili ya watu wake kupitia bwawa hilo la kuzalisha umeme barani Afrika. **RFI**

## Yaanza kumbukumbu mauaji kimbari

**Kigali,** RWANDA

NCHINI Rwanda imeanza maadhimisho ya miaka 27 ikiwa ni kumbukumbu ya mauaji ya kimbari.

Mwaka 1994 Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani, wakikadiriwa kufikia milioni moja waliuawa kwa kipindi cha siku 100.

Maadhimisho ya mwaka huu nchini Rwanda ambayo yameanza jana, yanafanyika tofauti na mwaka jana.

Hakukuwa na ratiba yoyote maalum kutokana na kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya corona, maofisa wachache watakusanyika kwenye eneo la Kumbukumbu ya Mauaji ya Kimbari ya Kigali, Gisozi kwa kuwasha moto wa matumaini.

Hafla ya kitaifa ilipangwa kufanyika katika uwanja wa Kigali na kukusanya maofisa na wawakilishi wa makundi ya watu tofauti, ikiwamo wanadiplomasia, manusura wa mauaji ya kimbari, wanawake, vijana, viongozi wa dini na sekta binafsi. Aidha, Rais Paul Kagame alitoa hotuba na shughuli zote zilizopangwa kufanyika, zilionyeshwa mubashara kupitia televisheni ya taifa.

Mauaji hayo ya Kimbari nchini Rwanda, yalianza Aprili 7, siku moja baada ya kudunguliwa kwa ndege ya aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Juvenal Habyarimana katika anga la uwanja wa ndege wa Kanombe, aliyeambatana na rais wa Burundi, Cyprien Ntaryamira na mawaziri wawili Cyriaque Simbizi na Bernard Ciza. **RFI**

## Mazungumzo kuhusu Iran yaanza

**Vienna,** AUSTRIA

IRAN, Urusi na Marekani zimeridhishwa na siku ya kwanza ya mazungumzo yanayonuiwa kuuokoa mkataba wa kimataifa, kuhusu mpango wa nyuklia wa Iran yaliyofanyika mjini Vienna, Austria.

Mkuu wa ujumbe wa Iran katika mazungumzo hayo, Abbas Araghchi alisema katika video iliyoonyeshwa kwenye runinga ya taifa Irinn, kwamba kwa ujumla mkutano ulifanyika vizuri.

Marekani haikuhudhuria mazungumzo hayo kwa sababu Iran ilikataa kukutana na ujumbe wa nchi hiyo, kutokana na vikwazo vilivyowekwa utawala wa mjini Tehran ambavyo bado havijaondolewa.

Balozi wa China katika UN, Wang Qun, aliitaka Marekani iiondolee vikwazo Iran na masharti dhidi ya kampuni na watu binafsi, wakiwamo wale wanaotokea China.

Akizungumza baada ya mkutano wa Vienna, Qun pia aliitaka Iran iheshimu kikamilifu mkataba wa mwaka 2015. **DW**

# CHELSEA, ARSENAL ZAMWANIA CALHANOGLU




**LONDON,** England

WAPINZANI wa jiji moja la London kwenye Ligi Kuu England, Arsenal na Chelsea zipo kwenye mbio moja ya kuwania saini ya nyota wa AC Milan, Hakan Calhanoglu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 anamaliza mkataba wake wa sasa msimu huu wa joto na anaonekana kuwa hajajiandaa kusaini mkataba mpya pale San Siro.

Kwa mujibu wa Sky sport Italia, Milan walimpa ofa ya mkataba mpya wa thamani ya euro milioni nne kwa mwaka ambao bila nafasi ya makubaliano zaidi, lakini nyota huyo anataka euro milioni tano.

Hali hii imevivutia klabu kadhaa ambazo zinahitaji huduma yake, Arsenal na Chelsea wakitajwa tayari wamefungua mazungumzo nae.

Licha ya ukweli kuwa klabu hizo zinaandaa malipo mazuri kwa nyota huyo, lakini wanatajwa kuwa bado hawajajiandaa kupambana na kiasi ambacho Juventus wanajiandaa kumlipa mchezaji huyo huyo.

Calhanoglu ametoa mchango wa pasi za mwisho nane na mabao mawili katika mechi 24 alizocheza msimu huu, na hadi sasa anaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kunasa kwenye windo la Juventus.

# Klopp: Tulirahisisha ushindi wa Madrid

**MADRID,** Hispania

JURGEN Klopp amesema Liverpool "walifanya urahisi sana" kwa Real Madrid kushinda mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini anahisi bao la Mohamed Salah limewapa maisha kuelekea mchezo wa marudiano kule Anfield.

Wekundu hao walionyesha kiwango cha kuvutia katika dakika za mwanzo na walikosa nafasi kadhaa za kufunga, kabla ya kupoteana.

Ghafla kibao kiliwabadilikia Liverpool baada ya Vinicius Junior kufunga bao la kwanza akiunganisha pasi ya Toni Kroos na Marco Asensio akafunga la pili kwa kosa la mlinzi, Trent Alexander-Arnold.

Liverpool walirudi mchezo na kuanza kutafuta mabao na Salah akifunga bao hilo la kufutia machozi.

Bao hilo limeifanya Liverpool kuwa na ahueni kuelekea mchezo wa marudiano utakaopigwa kwenye dimba la Anfield Aprili 14, mwaka huu.


"Kama unataka kwenda kwenye nusu fainali, unatakiwa kuwa na haki ya kufanya hivyo," alisema Klopp akiiambia BT Sport.

"Hatukufanya hivyo usiku wa leo (juzi), hasa katika kipindi cha kwanza.

"Hakutucheza kwa kiwango bora na hatukucheza mpira mzuri wa kuwapa matatizo Real Madrid. Tuliwarahisishia sana mambo.

"Kitu pekee kizuri ninachoweza kusema, kuacha bao tulilopata, tumemaliza nusu ya kwanza ya hatua hii.

"Hatukustahili zaidi, lakini bao moja na kiwango cha kipindi cha pili kilikuwa safi kwa upande wetu. Imetupa maisha kuelekea mchezo wa marudiano."






# Zidane azungumzia kuinoa Juventus

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesema "Juventus bado ni muhimu kwangu" wakati huu akihusishwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Kocha wa sasa wa Juventus, Andrea Pirlo amekalia kuti kavu pale Turin, ambapo timu yake ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Serie A na ikiwa hatarini kukosa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Juve na Cristiano Ronaldo waliondolewa hatua ya 16 na Porto kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kocha wa zamani, Massimiliano Allegri - ambaye aliondoka mwaka 2019 - amekuwa akihusishwa kurudi hapo baada ya kukutana na Rais, Andrea Agnelli.

Zidane alitumia miaka mitano akicheza pale Juventus, akishinda mataji mawili ya Serie A kabla ya kujiunga na Madrid mwaka 2001, na raia huyo wa Ufaransa, hakukataa uwezekano wa kurudi kwa Bianconeri hao.

"Zote, Italia na Juve ziko moyoni mwangu, nilitumia miaka mitano nikiwa Turin na Juventus bado ni muhimu kwangu," alisema Zidane akiiambia Sky Italia.

"Majaliwa ya baadaye Juve? Kwa sasa nipo hapa, tutaona hapo baadaye," aliongeza Zidane bada ya kuiongoza Madrid kushinda mabao 3-1 dhidi ya Liverpool kwenye mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne.

# Mandzukic kutemwa AC Milan

**MILAN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Mario Mandzukic, amekuwa akipambana na majeraha tangu aliporejea Italia na Rossoneri hao wameripotiwa hawana mpango wa kumwongezea mkataba mpya.

Nyota huyo wa zamani wa Juventus alirudi Serie A Januari, mwaka huu na alidhaniwa kuwa angeweza kumpunguzia jukumu kubwa, Zlatan Ibrahimovic kwenye safu ya ushambuliaji.

Mandzukic, aliyecheza mara 89 kwenye Timu ya Taifa ya Croatia, alichukua mataji ya Serie A manne na mataji matatu ya Coppa Italia wakati akiwa na Juventus.

Mchezaji huyo wa zamani wa Croatia alihamia Al-Duhail Januari 2020, lakini akarudi Serie A baada ya mwaka mmoja.

Lakini Kocha wa Milan, Stefano Pioli ameshindwa kumtumia mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Croatia kwa michezo 10, na mechi inayofuata dhidi ya Parma inaweza kuwa ya 11.

Tuttosport imeripoti Mandzukic anayo fursa ya kudhihirisha Milan kuwa wanakosea, ikiwa klabu kwa sasa haina nia ya kuongeza mkataba wake baada ya kiwango kisichoridhisha katika kurejea kwake Italia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amecheza michezo mitano ya ushindani kwa Milan na hajafunga bao akiwa na jezi ya kikosi hicho.

Alisaini mkataba wa miezi sita ambao unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.



# IBRAHIMOVIC APEWA MKATABA MPYA



**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic anatarajia kusaini mkataba mpya na AC Milan utakaomfanya kucheza kwenye viunga hivyo kwa mwaka mmoja zaidi hadi atakapofisha umri wa miaka 40.

Ibrahimovic anatarajia kufikisha umri huo Oktoba 3, mwaka huu, lakini hadi sasa hajaonyesha kushuka kiwango licha ya umri kumtupa mkono.

Kwenye Seria A msimu huu ameshafunga mabao 15 katika mechi 16 za michuano yote alizocheza na kuiwezesha timu hiyo kushika nafasi ya pili nyuma ya Inter Milan.

Sky Sports Italia imeripoti kwamba, baada ya uvumi uliokuwa unasambaa juu ya hatima yake mwisho wa msimu huu, viongozi wa Milan wamekaa naye na kufikia makubaliano ya kumwongeza mkataba wa mwaka mmoja.

Ripoti hiyo imeeleza kuwa dili hilo anatarajia kusaini ndani ya siku 10 zijazo kuanzia sasa.

Hata hivyo, hakutakuwa na mabadiliko ya mshahara anaopokea kwa sasa ambao ni pauni milioni 5.49 kwa mwaka.

Wachezaji wengine ambao Milan inatarajia kuwaongeza mikataba na mazungumzo bado yanaendelea ni golikipa wao namba moja, Gianluigi Donnarumma na kiungo kutoka Uturuki, Hakan Calhanoglu.

# *Hatima ya Nacho mikononi mwa Ramos*

**MADRID,** Hispania

MLINZI wa Real Madrid, Nacho Fernandez, amedokeza atasubiri kuona kama Sergio Ramos atasaini mkataba mpya kabla ya yeye kuamua kama atakubali pia masharti mapya.

Nahodha wa Madrid na Hispania, Ramos anapaswa kumaliza mkataba wake pale Santiago Bernabeu mwishoni mwa msimu huu, wakati Nacho ana msimu mwingine wa kukamilisha mkataba wake.

Madrid wamekuwa wakifanya mazungumzo na Ramos juu ya kuongeza muda wake wa kukaa hapo, lakini Kocha Mkuu Zinedine Zidane hivi karibuni alikiri kuwa hana hakika kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania atamwaga wino tena.


Hatima ya Nacho mwenyewe iko mbali na mtu huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye amekuwa akipangwa katika kikosi cha Zidane, ataona mipango ya Madrid ni nini kabla ya kufanya uamuzi wake.

"Kwa kweli, kama Madrid itamsainisha Ramos, au itasaini beki wa kati au wawili, ni uamuzi ambao unaathiri maisha yangu ya baadaye," alisema katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mechi Jumanne dhidi ya Liverpool.

"Ni kawaida, kila kitu kinaathirika, nitaiangalia, kuichambua na kuzungumza na klabu yangu na familia yangu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# USAJILI WA DYBALA JUVENTUS WAKWAMA

## ●●● Vigogo hao wa Italia hawako tayari kumwongeza ofa mpya au endapo nyota huyo...

**TURIN,** Italia

HATIMA ya nyota wa Juventus, Paulo Dybala bado inaendelea kuwa na sintofahamu baada ya kibibi kizee hicho cha Turin, kujiondoa kwenye mazungumzo ya nyongeza ya mkataba wake.

Mkataba wa sasa wa Dybala wa euro milioni 7.5 kwa mwaka unamalizika Juni, mwakani na Juventus tayari walikuwa wamekaa mezani kwa ajili ya mkataba mpya wenye thamani ya euro milioni 10 kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Sky Sport Italia, Dybala na wawakilishi wake wamekataa ofa ya euro milioni 10 na wanataka euro milioni 15 kwa mwaka.

**Sky Sport Italia kupitia mtandao wa Calciomercato.com imeripoti kwamba, Juventus wameamua kuondoa ofa yao hiyo ya mwisho mezani.**

Suala hili linakuja ikiwa ni baada ya Dybala na wenzake kuvunja taratibu za kujikinga na corona wiki iliyopita kwa kuhudhuria hafla binafsi nyumbani kwa Weston McKennie.

Wakati Juventus ikifanya uamuzi wa kuwalipisha faini, huku Andrea Pirlo akiwaondoa kwenye kikosi cha kupambana na Torino wikiendi iliyopita, Dybala anatajwa kuwa amepata madhara zaidi baada ya tukio hilo.

Uamuzi wa Juventus ni kuwa hawapo tayari kumpa ofa mpya, na ikiwa nyota huyo anataka kuongeza mkataba basi atafanya hivyo kwa ofa ya mkataba wake wa sasa, malipo na masharti yakiwa ni yale yale.

## ZISIKUPITE

### AGUERO KUBAKIA EPL

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Sergio Aguero, 32, yuko tayari kukosa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, ili abakie kwenye Ligi Kuu England, huku Chelsea na Tottenham Hotspur zikiwa miongoni mwa klabu atakazozifikiria. ***(Telegraph)***

### UNITED YAMTAKA KONATE

MANCHESTER United inaweza kujiunga na Liverpool katika mbio za kuwania saini ya mlinzi wa kati wa RB Leipzig, Ibrahima Konate, 21. Mchezaji huyo anatajwa thamani yake kuwa ni pauni milioni 34. ***(Eurosport)***

### WEST NA LINGARD

KLABU ya West Ham itajaribu kumsajili kiungo wa kati, Jesse Lingard, 28, kwa mkataba wa kudumu mwishoni mwa msimu huu, lakini wanahofia Manchester United watataka dau la juu ili kumwachia mchezaji huyo. ***(Mail)***

### LACAZETTE KUUZWA

ARSENAL itafikiria kumuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Alexandre Lacazette, 29, katika dirisha la usajili katika majira ya joto. Inter Milan, Roma, Sevilla na Atletico Madrid zimeonyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo. ***(90min)***

### SABITZER SOKONI

KLABU ya Tottenham Hotspur inajiandaa kumsajili kiungo wa kati wa RB Leipzig, Marcel Sabitzer mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

### CALHANOGLU AGOMBEWA

KLABU za Juventus, Arsenal na Chelsea zinamtolea macho kiungo wa kati wa AC Milan, Hakan Calhanoglu mwenye umri wa miaka 27 raia wa Uturuki, ambaye anaweza kupatikana kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Sports)***

### MORENO BEI JUU

MSHAMBULIAJI wa Villarreal, Gerard Moreno, 28, ametajwa kuwa gharama yake ya usajili ni pauni milioni 85.6 kwa timu yoyote itakayomtaka. ***(Marca)***

### WALCOTT MAMBO SAFI

STRAIKA, Theo Walcott, 32, atajiunga na Southampton kwa mkataba wa kudumu, mara mkataba wake wa kucheza kwa mkopo Everton utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Talksport)***

### EVERTON KUMUUZA MINA

KLABU ya Everton itahitaji kiasi cha pauni milioni 21.4 kwa mlinzi wao wa kati, Yerry Mina. ***(Team Talk)***

### DEMBELE HAONDOKI

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amemtaka mshambuliaji, Ousmane Dembele, 23, kubakia klabuni hapo, licha ya Manchester United kuonyesha nia ya kutaka kumsajili raia huyo wa Ufaransa. ***(Metro)***

## Namungo, Ihefu FC zatishana Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

NYASI za viwanja viwili zinatarajia kuwaka 'moto' katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo Namungo FC itawakaribisha Ihefu FC kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa wakati Mbeya City itawavaa Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na kikosi kipo tayari kukabiliana na wapinzani wao kutoka jijini Mbeya.

Morocco alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani kwa sababu timu zote zinahitaji kupata matokeo chanya ili kujiweka katika nafasi nzuri ya uhakika wa kubakia kwenye ligi hiyo.

"Hautakuwa mchezo rahisi, kwa sababu kila mmoja wetu anatafuta matokeo mazuri, tutaingia uwanjani kwa kuwaheshimu wapinzani wetu, tuko nyumbani tunahitaji kutumia vizuri uwanja wa nyumbani, pia wenzetu wanatafuta matokeo mazuri," alisema Morocco.



Naye Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila (pichani) alisema wanahitaji pointi tatu muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea kubaki katika ligi hiyo.

Katwila alisema timu yake iko katika nafasi mbaya kwa sasa wanahitaji kupambana zaidi ili kuondoka na pointi tatu na hatimaye kujinasua kwenye nafasi waliyopo kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Nimewaambia wachezaji wanapaswa wajiamini na tupambane kuhakikisha tunapata pointi tatu kwenye mechi zetu zilizobakia ikiwamo dhidi ya Namungo FC, haitakuwa rahisi ukizingatia kila timu kwa sasa inahitaji pointi," alisema Katwila.

# WAAMUZI WATIA NENO, LIGI KUU BARA IKIREJEA

**Na Adam Fungamwango**

WAKO tayari! Hayo ni maneno kutoka katika Kamati ya Waamuzi kuelekea hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inarejea rasmi leo kwenye Uwanja wa Sokoine kwa Mbeya City kuikaribisha Kagera Sugar huku kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Namungo FC ikiwaalika Ihefu FC.

**Mwenyekiti wa Kamati wa Waamuzi, Soudi Abdi, aliliambia gazeti hili waamuzi wamejiandaa vyema kuchezesha mechi za ligi hiyo na akizitaka timu zote kuingia uwanjani kucheza mpira na si kwenda na matokeo mfukoni.**

"Waamuzi wako tayari. Ligi inaendea mwishoni, kuna timu ziko juu ya msimamo zikisaka ubingwa na nyingine zinaepuka kushuka daraja, hivyo waamuzi wanakwenda kukabiliana na changamoto hizo, kuna baadhi ya timu ambazo zikishindwa zinatafuta sababu wakati mwingine si za kweli, lakini tumejiandaa," alisema Abdi.

Kuhusu dosari za waamuzi, mwenyekiti huyo alisema haiwezekani kutokuwapo kabisa kwa sababu hata kwenye ligi mbalimbali Ulaya ambapo kuna teknolojia za kisasa, lakini makosa au dosari zinakuwapo tu, lakini watakachofanya ni kuzipunguza kwa kiasi kikubwa.

"Ujue wanaochezesha ni binadamu, dosari ndogo zitakuwapo tu, ila waamuzi watajitahidi sana kuchezesha kwa haki, na hata zikitokea kama timu imejiandaa kucheza soka, itaona kuwa ni za kibinadamu tu. Mimi nazikata timu zikacheze mpira. Ukiingia na mawazo ya kuonewa kila kitakachotokea utaona unaonewa tu," Abdi alisema.

Mara ya mwisho mashabiki kushuhudia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni Machi 14, mwaka huu ambapo Prisons waliwakaribisha JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga na wenyeji waliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Mbeya City inaivaa Kagera Sugar ikiwa kwenye nafasi ya 16 na pointi 20 mkononi huku wageni wao wakiwa nafasi ya 13 kwa kukusanya pointi 25.

Namungo iko kwenye nafasi ya 10 kwa pointi 27 wakati huku Ihefu ikiwa kwenye nafasi ya 17 kwa pointi 20.

Yanga yenye pointi 50 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na watani zao na mabingwa watetezi, Simba ambao wana pointi 46 lakini wakicheza mechi tatu pungufu.



Kocha wa makipa wa KMC FC, Fatuma Omary (kulia), akiwafundisha magolikipa wa timu hiyo kwa ajili ya maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hababuu kocha mpya wa Zanzibar Heroes

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limemteua Hababuu Ali Omar kuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) itakayoshiriki mashindano ya Kombe la CONIFA Afrika ambayo yatafanyika visiwani hapa ifikapo Mei, mwaka huu.

Hababuu amechukua nafasi ya Hemed Suleiman 'Morocco' ambaye alikuwa akikinoa kikosi hicho kwa muda mrefu.

Kaimu Katibu Mkuu wa ZFF, Haji Hassan 'Kibabu' alisema katika majukumu hayo mapya, Hababuu atasaidiwa na Sheha Khamis huku Mohamed Abassi Silima atakuwa kocha wa magolikipa na viongozi wengine wa timu hiyo watatangazwa baadaye.

"Kwa sasa tumetangaza makocha tu ambao watakinoa kikosi cha Zanzibar Heroes kuelekea michuano hiyo ya CONIFA, muda si mrefu watakabidhiwa majukumu yao, halafu ndio watangaza benchi lao lote pamoja na kikosi cha timu hiyo kitakachoshiriki mashindano hayo,"alisema Kibabu.

Bingwa wa michuano hiyo atakata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia ya CONIFA kutoka Afrika inayotarajia kuchezwa mwakani nchini Kurdi Stan.

Michuano hiyo ya CONIFA Afrika inashirikisha nchi za Afrika ambazo si wanachama moja kwa moja wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) na lile la Afrika (CAF).

# Michezo

Alhamisi Aprili 8, 2021

Nipashe




Usajili wa Dybala Juve wakwama UKURASA 22





Kiungo wa Real Madrid, Marco Asensio, akifunga bao baada ya kumpiga chenga golikipa wa Liverpool, Alisson (hayupo pichani), na kumtoka beki wa timu hiyo, Trent Alexander-Arnold (kushoto), katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku. Madrid ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba kufunga hebabu kibabe

**Na Saada Akida**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wakiwasili salama jijini Cairo, beki wa timu hiyo, Mkenya Joash Onyango, amesema wamekwenda nchini Misri kwa lengo la kupambana kusaka ushindi dhidi ya wenyeji Al Ahly na si kukamilisha ratiba.

Al Ahly inatarajia kuwakaribisha Simba katika mechi ya mwisho ya Kundi A itakayochezwa kesho huku timu hizo mbili tayari zikiwa zimefuzu kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuondoka nchini juzi, Onyango alisema licha ya timu yao kufuzu hatua inayofuata, hawatabweteka katika mchezo huo wa mwisho dhidi ya vigogo hao wa Afrika.

Onyango alisema ubora unaoonyeshwa na kikosi chao unatokana na malengo waliyojiwekea pamoja na umoja waliokuwa nao ndani ya timu hiyo ambayo pia inashikilia taji la Ligi Kuu Tanzania Bara.

Beki huyo aliongeza wamefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya mchezo huo na watahakikisha kila mmoja anatimiza majukumu yao ili kupata matokeo chanya katika mchezo huo utakaochezwa kuanzia saa 4:00 usiku.

"Hautakuwa mchezo rahisi, tutacheza kwa tahadhari na nidhamu ya hali ya juu, kwa sababu Al Ahly ni timu nzuri, inahitaji kufanya vizuri nyumbani kwao, hata sisi tumejipanga kutafuta matokeo mazuri ugenini,"alisema Onyango.

# Ntibazonkiza: Yanga itang'ara

### ●●● Yajipanga kurejea na kasi pamoja na nguvu mpya ili kumaliza...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Yanga kikitarajia kurejea uwanjani keshokutwa kuendelea na mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa timu hiyo, Saido Ntibazonkiza amesema mashabiki wasiwe na hofu kwa sababu nia na nafasi ya kutwaa ubingwa wanao.

**Yanga inatarajia kushuka dimbani keshokutwa kuwakabili KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ntibazonkiza alisema hakuna timu wanayoihofia katika ligi hiyo inayokaribia ukingoni na kila siku kikosi chao kinajiimarisha ili kusaka pointi tatu kwenye kila mechi watakayocheza.

Ntibazonkiza alisema mashabiki na wanachama wa timu hiyo wasiwe na wasiwasi kwa sababu wachezaji wote wamejipanga kupambana katika kila mechi ili kujiimarisha kwenye uongozi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Nyota huyo alisema anaendelea vizuri na mazoezi na amepewa programu maalum kabla ya baadaye kuungana na wachezaji wenzake katika mazoezi ya pamoja.

"Ninaamini nitakuwa na kipindi kingine kizuri, kwa sasa niko fiti, ninamshukuru Mungu, mengine yataonekana kwa vitendo uwanjani, kikubwa ni kuwa na afya njema," alisema kiungo huyo ambaye awali kabla ya ligi haijasimama alikosekana ndani ya kikosi cha Yanga kwa muda wa zaidi ya mwezi mmoja kutokana na kuguza maumivu ya nyonga.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, aliliambia gazeti hili anaamini kikosi chake kitaendelea kupata matokeo chanya katika mechi zake tano zinazofuata ambazo zitachezwa hapa jijini.

Mwambusi alisema Yanga imekuwa na rekodi nzuri kwenye uwanja huo na mapumziko yaliyomalizika waliyatumia kurekebisha upungufu mbalimbali na sasa watarejea na nguvu mpya.

"Timu inaendelea vizuri na maandalizi kuelekea mchezo wa ligi dhidi ya KMC, tunajua mechi haitakuwa rahisi, tunakutana na moja ya timu zinazotoa ushindani na zenye rekodi nzuri pia, wachezaji wote wako vizuri na wanaendelea kujiimarisha, Saido ameshaanza mazoezi lakini alikuwa katika programu maalum," alisema Mwambusi.

Aliongeza kikosi cha Yanga kimeendelea kuimarika na kiu ya mafanikio ambayo kila mchezaji anayo, inasaidia kuongeza ubora wa timu.

"Kila mmoja anataka kuonyesha wamedhamiria kusaka ubingwa, ushindani unaonekana mazoezi ni dalili nyingine nzuri za kuelekea kwenye mafanikio, utulivu na umakini ukiwepo, hakika tutafikia kile tunachokihitaji," Mwambusi alisema.

Baada ya mechi hiyo ya keshokutwa, Yanga itaendelea kubakia jijini kucheza dhidi ya Biashara United ifikapo Aprili 17, mwaka huu na siku tatu baadaye itawaalika Gwambina FC wakati Aprili 23, mwaka huu wataivaa Azam FC huku mchezo wake wa nne mfululizo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >